# Nipashe

Jumanne Septemba 24, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581809

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper


UKURASA 2

**Vituo** 300 Kiswahili kujengwa ughaibuni



UKURASA 2

**Vibanda** 3,000 vya biashara soko la Machinga vyateketea moto

UKURASA 7

**SMZ** kujenga hospitali kubwa ya rufani mkoa Kaskazini Unguja



**HAALAND AFIKIA REKODI YA RONALDO MADRID**

UKURASA 22

MAANDAMANO CHADEMA

# Polisi yayadhibiti, yakiri kukamata 14

UK. 3



Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, akiwa chini ya ulinzi wa polisi alipokamatwa eneo la Magomeni Mapipa Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA NA JENIFER GILLA**

**MICHEZO** **FADLU: SIMBA BADO, ITAKUWA TISHIO ZAIDI** UK.24

**KATUNI** UK.6

# Samia: Serikali, diaspora kufungua vituo 100 vya Kiswahili duniani

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema serikali kwa kushirikiana na Watanzania waishio nje ya nchi (diaspora) wamepanga kufungua vituo 100 vya lugha ya Kiswahili kwenye maeneo mbalimbali duniani.

Aidha, vijana wabunifu wametakiwa kutumia mbandiko (Application) mbalimbali kwa ajili ya kufundisha Kiswahili kupitia mitandao ambayo itawafikia wananchi wengi.

Samia alitoa kauli hiyo jana, akifunga kilele cha Tamasha la Kitaifa la Utamaduni lililofanyika katika mji wa Songea, mkoani Ruvuma, akiwataka Watanzania waishio nje pamoja na vijana, kuchangamkia fursa zitakazopatikana kupitia lugha hiyo.

Aliwataka vijana watumie ubunifu kwa kutengeneza maigizo na teknolojia nyingine ili kuyafikia mataifa mengine kujifunza Kiswahili ambacho kwa sasa kinatoa ajira na fursa mbalimbali za kiuchumi.

Aidha, alisema njia nyingine ya kusaidia lugha hiyo ni kutambulika zaidi duniani na vyuo vikuu nchini kushirikiana na vyuo vya nje kuhamasisha kutumia lugha hiyo.

"Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo imenijulisha kwamba mwaka huu imepanga kufungua vituo 100 vya Kiswahili kote duniani kwa kushirikiana na diaspora yetu, niwatake Watanzania waliopo nje ya nchi kuchangamkia fursa ya kufundisha Kiswahili, pia vijana kupitia ubunifu wa maagizo na mtandiko watu watavutika kutaka kuifahamu lugha hiyo nanyi mtajiingizia kipato alisema," alisema. Katika hatua nyingine, Rais Dk. Samia, aliiagiza Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo kuandaa mapendekezo ya kushughulika na masuala ya mmomonyoko wa maadili.

Alisema mapendekezo ya wizara yataisaidia serikali jinsi ya kupambana na mmomonyoko wa maadili ambao alisema umetokana na mwingiliano wa utamaduni wa kigeni na kuwataka wazazi na walezi kukagua mwenendo na maadili ya watoto wao.

Awali, Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Damas Ndumbaro, alimweleza Rais Samia kuwa ni msimu wa tatu Tamasha la Kitaifa la Utamaduni linafanyika na kwa mara ya kwanza lilikuwa Septemba 8, 2021, la pili lilifanyika mkoani Njombe na sasa limefanyika Ruvuma.

Alisema tamasha hilo linajitahidi kutimiza falsafa za Rais Samia ambazo ni maridhiano kwa kuhusisha makabila yote kubadilisha mawazo na kutatua migogoro katika sekta ya utamaduni, sanaa na michezo kwa kuzingatia maridhiano.

Kuhakikisha sekta ya michezo inachangia Pato la Taifa kutoka asilimia 0.4 hadi kufikia nne, kujenga upya, kutetea maadili na kukuza sekta ya muziki na sanaa.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, alisema wamenufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile sekta ya afya, kilimo, elimu na nishati, hadi sasa zaidi ya vijiji 500 vimeunganishwa na umeme.

Rais Samia ambaye ameanza ziara ya siku sita mkoani Ruvuma kwa ajili ya kukagua miradi ya maendeleo, alisema kuwa tangu iingie madarakani mwaka 2021 serikali imetoa fedha nyingi kujenga shule, hospitali, maji, barabara, kuboresha sekta ya madini na kilimo.

Alisema ameridhishwa na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Songea kilichogharimu Sh. bilioni 40.

Pia, kiwanja hicho kimeboreshwa na kina uwezo wa kushusha abiria kutoka 3,000 katika mwaka 2021 hadi kufikia 1920, mwaka huu.

**Imeandikwa na Grace Mwakalinga (DAR) na Gideon Mwakanosya (RUVUMA)**



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwapungia mkono viongozi mbalimbali pamoja na wananchi baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Songea, mkoani Ruvuma jana. **PICHA: IKULU**

## Walioshtakiwa kubaka kwa kundi wakutwa na kesi ya kujibu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Dodoma, imewakuta na kesi ya kujibu washtakiwa wanne wa kesi ya kubaka kwa kundi na kumwingilia kinyume na maumbile binti mkazi wa Yombo Dovya, jijini Dar es Salaam.

Washtakiwa hao wamekutwa na kesi ya kujibu jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama hiyo, Zabibu Mpangule na watatakiwa kujitetea kuanzia kesho.

Upande wa Jamhuri ulileta jumla ya vielelezo 12 na mashahidi 18 ambao walitoa ushahidi kuhusu kesi inayowakabili washtakiwa hao ambao ni askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Clinton Damas, maarufu Nyundo, askari Magereza, Praygod Mushi, Nickson Jackson 'Machuche' na Amin Lema anayejulikana pia kwa jina la Kindamba.

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya Mahakama jana, wakili wa washtakiwa hao, Godfrey Wasonga, alisema mahakama imetoa uamuzi kuwa washtakiwa wote wana kesi ya kujibu na wanatakiwa kujitetea kuanzia kesho na wao wameshajipanga.

# Vibanda 3,000 biashara soko la Machinga vyateketea kwa moto

**Na Vitus Audax,** MWANZA

ZAIDI ya vibanda 3,000 vya wafanyabiashara wadogo, maarufu kama Machinga katika Soko la Ukwaju, vimeteketea kwa moto ambao uliwaka kwa zaidi ya saa tano huku chanzo kikiwa bado kinachunguzwa.

Wakizungumza na Nipashe katika eneo hilo maarufu kama Bango la Zain, baadhi ya mashuhuda na wafanyabiashara wenye vibanda walisema moto huo ulizuka majira ya saa 2:00 asubuhi huku Jeshi la Zimamoto na Uokoaji likishindwa kufika kwa wakati kutokana na gari kupata ajali.

Mmoja wa mashuhuda, Bahati Gavani, alisema katika soko hilo kulikuwa banda moja ambalo halitumiki lililokuwa na nyuki na kwamba kulikuwa na viashiria kulikuwa na watu wanarina asali kwa kutumia moto.

"Hao nyuki walikuwapo kwa muda mrefu katika banda hilo lililotengenezwa kwa dari (ceiling board), hivyo wakati soko linaungua, tuliona kama kulikuwa na mtu anavuna asali kwenye banda hilo," alisema Gavani.

Mfanyabiashara Naomi Shema alisema vibanda hivyo walivijenga kutokana na agizo la serikali kuwataka kutoka maeneo yasiyo rasmi na kuwa waliyajenga kwa mikopo ambayo bado wanailipa.

Kuhusu bidhaa, Shema alisema kwenye vibanda hivyo hakukuwa na bidhaa kutokana na wafanyabiashara hao kurejesha shughuli zao katika maeneo walikoondolewa awali kutokana na kukosa huduma muhimu sokoni hapo.

"Tunaomba serikali itusaidie kurejesha miundombinu ya vibanda vyetu kwani kwa sasa hatuna uwezo kabisa wa kuvijenga tena kwa sababu mikopo yenyewe tulikopa ili kuvijenga bado hatujakamilisha urejeshwaji wake," alisema Debora Omary.

Mwenyekiti wa Soko hilo, John Paulo alisema soko hilo lilianzishwa Oktoba, 2021 kutokana na maelekezo ya Rais kuwa Machinga wapangwe na kuondolewa katika maeneo yasiyo rasmi na wengi waliitikia agizo hilo.

"Hapo kila banda lilijengwa kwa gharama za wastani wa Sh. 360,000 lakini kutokana na kutokuwapo kwa baadhi ya huduma muhimu na wateja, wafanyabiashara walirejea katika maeneo yao ya awali," alisema Paulo.

Alisema baada ya kutokea kwa moto huo, walijulishwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambao wakati wanakwenda katika tukio hilo, gari lao lilipata ajali kisha kutumwa lingine ambalo lilifika kwa kuchelewa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Naibu Kamishna (DCP) Wilbroad Mutafungwa, alisema katika tukio hilo hakuna majeruhi wala kifo kwa kuwa hakukuwa na watu katika eneo hilo.

"Tulipopata taarifa hiyo tulifika na kukuta tayari moto ni mkali na kushirikiana na wananchi waliokuwapo kuudhibiti wakati tukawajulisha wenzetu wa zimamoto. Hakuna mtu aliyepoteza maisha wala aliyejeruhiwa na vibanda vichache vya barabarani vilivyokuwa na mali wafanyabiashara walijitahidi kuziondoa," alisema.

Pia alisema vibanda vingi havikuwa na mali na kuwa walishirikiana na Shirika la Umma Tanzania (TANESCO) ambao waliwahi kukata umeme ili kudhibiti madhara zaidi.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Mutafungwa alisema kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wanaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo huku akiwaonya wananchi kutokuingia katika eneo hilo kwa ajili ya usalama wa mali za wafanyabiashara, yakiwamo mabati.

HABARI KITAIFA

# Polisi yadhibiti maandamano CHADEMA

Na Waandishi Wetu

JESHI la Polisi nchini limefanikiwa kudhibiti maandamano ya viongozi na wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) katika maeneo mbalimbali Dar es Salaam.

Aidha, Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alitaja viongozi na wanachama 14 waliokuwa wanashikiliwa kwa madai ya kukaidi katazo la polisi la maandamano lililotolewa Septemba 12, mwaka huu.

Kamanda Muliro alisema jana kuwa mwezi huu, viongozi na wanachama wa CHADEMA walitoa matamko mbalimbali yenye viashiria vya uvunjifu wa amani na kujenga hofu kwa wananchi na kwamba walipanga kufanya maandamano jana ambayo yalipigwa marufuku na polisi.

Aliwataja walioshikiliwa kuwa ni Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, Makamu Tundu Lissu, na Mwenyekiti wa Kanda ya Kaskazini na Mjumbe wa Kamati Kuu, Godbless Lema.

Wengine ni Peter Lazaro, Sheikh Omari Fakhi, Revocatus Mlay, Paulo Musisi, Shabani Kinde, Abubakar Mugalu, Emmanuel Ntobi, Sylvester Satu, Rachel Mlondela, Mary Nungi na Bakari Salum.

**TAARIFA YA CHADEMA**

Kutokana na tukio hilo, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alitoa taarifa kuwa viongozi wanane, walinzi na watumishi wa makao makuu waliokuwa ofisini na zaidi ya wanachama 40 wanashikiliwa na polisi.

Aliwataja wengine ambao hawatajatwa kwenye taarifa ya polisi kuwa ni Naibu Katibu Mkuu, Benson Kigaila, Mke wa Mbowe, Dk. Lilian Mtei, wakili na mtoto wa kiongozi huyo, Nicole Mbowe aliyekuwa ameongozana na baba yake.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mrema, wengine waliokamatwa ni wenyekiti wa mikoa ya Katavi na Shinyanga Rhoda Kunchela na Emmanuel na viongozi mbalimbali wa majimbo ya Kanda ya Pwani.

"Tunatoa wito kwa Jeshi la Polisi kuheshimu katiba na sheria za nchi kwa kuwa kuandamana si kosa kwa mujibu wa katiba, sheria na taratibu zilizopo. "Pia tunalitaka Jeshi la Polisi kuheshimu haki zote za waliokamatwa na kuwatendea kama watu ambao si wahalifu kwa wakati wote wa kushikiliwa kwao," alisisitiza.

Awali, alisema chama hicho kilitangaza kuwa jana ingekuwa siku ya maombolezo juu ya viongozi, wanachama na wananchi mbalimbali ambao wametekwa, kuteswa, kuumizwa, kupotezwa na wengine kuuawa nchini.

"Pamoja na kufuata utaratibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa kifungu Cha 11(4) kuhusu kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi juu ya maandamano ya amani ambayo yalipangwa kufanyika Dar es Salaam. Polisi wameamua kutumia nguvu kupita kiasi kudhibiti maandamano hayo," alisema Mrema.

**WAANDISHI WAKAMATWA**

Waandishi watano na wapigapicha wa magazeti ya Nipashe, Mwananchi, walikamatwa na polisi katika maeneo mbalimbali wakitekeleza majukumu yao kwenye matukio ya maandamano.

Mpigapicha Jumanne Juma alikamatwa Kituo cha Mafuta Buguruni wakati akipiga picha wanachama wa CHADEMA waliokusanyika eneo hilo.

Baada ya kukamatwa, alipelekwa Kituo cha Polisi Buguruni, ambako alihojiwa kwa saa moja kwamba kwa nini anapiga picha wakati hakuna maandamano.

"Nilipofika nilikwenda kujitambulisha kwa kiongozi wa askari waliokuwapo lakini baada ya muda walituzunguka wakatukamata mimi na mwandishi wa Mwananchi. Tukapelekwa kituoni tukahojiwa, baadaye wakatupeleka kwa mkuu wa kituo ambaye aliwaambia kama wametuhoji na hatuna madhara tuachiwe ndipo tukaachiwa," alisema Juma.

Aidha, Mwandishi wa Nipashe, Jenipher Gilla, alikamatwa wakati akikusanya taarifa za maandamano hayo kisha kupelekwa Kituo Kikuu cha Polisi.

Akizungumza kituoni hapo, alisema alifikishwa kisha kuhojiwa kwa nini alikuwa anakusanya taarifa kwenye eneo hilo. Waandishi wengine waliokamatwa ni Michael Matemanga na Lawrence Mnubi wa Mwananchi na Mariam Shaban wa EATV.

**WAANDISHI KUFUKUZWA**

Baada ya zogo la mwandishi, Mbowe na makada kutamatika palitulia kwa muda eneo hilo ilipofika majira ya saa 6:45 adhuhuri, Jeshi la Polisi lilianza kuwafukuza waandishi eneo la Magomeni Mataa ambako kamatakamata hiyo ilikuwa ikifanyika na kuamuru waende wakakae upande wa pili uliko Msikiti wa Kichangani.

Hata hivyo ulitokea ubishani mkali waandishi wakidai wananyimwa uhuru wa kuripoti maandamano hayo japo majibu ya Polisi yalikuwa "hapa hamna jipya tena mmeshaturekodi sana inatosha."

Ubishani huo ulidumu kwa dakika kadhaa mpaka alipotokea mmoja wa askari ambaye aliwaondoa na kuwapeleka nyuma ya kituo cha mafuta ambako isingekuwa rahisi kuona kinachoendelea mbele ya barabara.

**HALI ILIVYOKUWA**

Mbowe alifika eneo la Magomeni majira ya saa 4:00 asubuhi, kuangalia usalama wa eneo kwa kuwa ndipo maandamano yalipangwa kuanzia. Kabla ya kufika eneo hilo, tayari askari polisi walikuwa wametanda kuanzia Magomeni Mataa, Mapipa hadi Usalama.



Mawakili wa Boniphace Jacob, Peter Kibatala (kushoto) na Dickson Matata, wakitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam jana baada ya kesi inayomkabili mteja wao kuahirishwa kutokana na hali ya kiusalama. Mahabusu wote katika mahakama za Dar es Salaam hawakuletwa mahakamani jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

Mbowe alifika eneo hilo pasi na Polisi na waandishi waliokuwapo baada ya kujua amefika akiwa katika gari ndogo, alimshtua mmoja ili awaite wengine azungumze nao. Wakati mazungumzo yakiendelea, polisi walimfuata na kumkamata huku wakimweleza aingie kwenye gari waondoke.

Kabla ya kukamatwa, Mbowe aliwaambia waandishi wa habari kuwa maandamano hayo ni ya amani na lengo lao ni kuomboleza vifo vya makada wa chama hicho na kukemea mauaji na utekaji.

"Hapa ndio tulipanga kuanzia maandamano yetu, maandamano yetu ni ya amani na hatuna nia ya kudhuru watu wala serikali. Kuna madai tuliyatoa kwa serikali hayajafanyiwa kazi, maandamano ni haki yetu kikatiba pale nguvu kubwa kama hii inavyotumika kukusanya askari wenye silaha na gharama kubwa kwa kutumia kodi za wananchi hii haiko sawa.

"Nimelazimika kuja hapa Magomeni na niko tayari kwa lolote maandamano haya si ya CHADEMA tu bali kwa mtu yoyote anayechukizwa na vitendo vya mauaji na utekaji," alisema Mbowe.

Wakati Mbowe anamalizia kauli yake maofisa wa Jeshi la Polisi walivamia mahojiano yake na kuanza kumzonga wakitaka aingie kwenye gari. Zogo hilo lilidumu kwa dakika kadhaa kisha Mbowe akashindwa kihimili mkikimikiki na kukubali kuingia katika gari dogo jeusi.

Wakati anapeleka kuingizwa katika gari hilo alikuwa akitamka kwangu: "Haya ndiyo malipo ya kutetea demokrasia na mauaji, hii ndio gharama tunayolipwa katika nchi."

Katika eneo la Mnazi Mmoja, ambako maandamano yalipangwa kupokewa yakitokea Magomeni na Ilala Boma, hali ilionekana kuwa shwari kuanzia majira ya saa 1:00 asubuhi wakati jua likichomoza hadi 7:00 mchana, huku kelele za magari na shughuli mbalimbali za wananchi zikitawala.

Katika barabara inayotoka Ilala Boma hadi Mnazi Mmoja, askari walionekana kutanda maeneo mbalimbali kama Karume na Kariakoo, huku kwa upande wa Magomeni walionekana Jangwani na Fire kuelekea katikati ya mji.

**MAONI YA WANANCHI**

Mwanaharakati Helen Kijo Bisimba alisema: "Nilikuwa bado natafakari kuwa kama taifa hatutaki kuingiliwa mambo yetu ya ndani, nikakumbuka tulivyokuwa mstari wa mbele kukemea yaliyokuwa yanaendelea Afrika Kusini kwa makaburu, Rodesia ya Kusini na Kaskazini hadi Nigeria kule Biafra yale hayakuwa mambo ya ndani ya nchi zile?

"Tumefika mahali na sisi tunatenda mambo ambayo wengine hawawezi kunyamaza. Wapo wanaoingilia mambo yetu ya ndani kwa kujenga zahanati ambazo ni kazi zetu hatukuwakataza, ila wakituonyesha ukweli wa maovu ya ukiukwaji haki, tunadai wanaingilia mambo yetu ya ndani. Tujirudi serikali ifanye masahihisho badala ya kulaumu wanaowaambia ukweli."

Richard Mabala aliandika: "Serikali ilipewa wiki moja kujikita katika kuondoa sababu ya maandamano kwa kuonyesha umakini katika kukomesha utekaji na kuwakamata watekaji au kujikita katika kuzuia maandamano kwa mabavu ya kila aina, inasikitisha sana kwamba waliamua kujikita katika ya pili."

Manyerere Jackton aliandika: "Hutakiwi kuwa mfuasi wa chama cha upinzani kuamini kuwa maandamano ya amani ni haki ya kiraia, na kwamba kuandamana ni sawa na kufungua chupa iliyojazwa chai ya moto!

"Watu wakiandamana wanapumua. Hakuna sababu ya kutumia gharama kubwa kuzuia haki za kiraia, maandamano ya kweli hayapo barabarani bali yako vichwani na mioyoni mwa watu, je, nani wa kuyazuia maandamano yaliyo mioyoni mwa watu? Tuione na tuifanye Tanzania kuwa ni yetu sote Amani Daima."

Imeandikwa na Halfani Chusi, Maulid Mmbaga, Jenipha Gilla na Grace Mwakalinga.

# Boniface kuendelea kusota rumande hadi Septemba 26

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Meya wa Ubungo, Boniface Jacob maarufu kwa jina la 'Boni Yai' ameendelea kusota rumande, baada ya kushindwa kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kwa ajili ya kusomewa uamuzi wa pingamizi la dhamana yake.

Aidha, mahabusu wote wa gerezani hawakufikishwa mahakamani jana.

Kesi hiyo ilipangwa kutolewa uamuzi jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Franco Kiswaga wa mahakama hiyo, lakini imeahirisha hadi Septemba 26.

Awali, upande wa mashtaka uliwasilisha maombi mawili mbele ya mahakama hiyo ikiwamo kupinga Jacob kupewa dhamana katika mashtaka mawili yanayomkabili likiwamo la kuchapisha taarifa za uongo.

Katika maombi yao wanaiomba mahakama itoe amri kwa mujibu maombi kuruhusu kupekuliwa akaunti yake ya X na kutoa nywila (password), ili kurahisisha uchunguzi wa akaunti hiyo inayoendana na makosa yake.

Ombi la pili la upande wa mashtaka, waliiomba mahakama kutotoa dhamana kwa mshtakiwa (Jocob) kwa sababu za usalama wake akiwa uraiani.

Kosa la kwanza anadaiwa kuchapisha taarifa za uongo, Septemba 12, kuwa Mafwele anatuhumiwa na familia nyingi kwa kupotea.

Kosa la pili, ambalo lilitokea Septemba

14, 2024, linahusiana na kuchapisha taarifa nyingine za uongo zinazosomeka 'Polisi wanatesa watu na kuua ndio kazi wanaweza.

Hata hivyo, Boniface alikana mashtaka yote hayo na upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Nasoro Katuga uliwasilisha maombi hayo mawili ambayo yalitakiwa kutolewa uamuzi wake jana.

Septemba 19, 2024 Jacob alipandishwa kizimbani na kusomewa mashtaka ya kuchapisha taarifa za uongo, jopo la mawakili wa serikali liliwasilisha hoja ya kutaka anyimwe dhamana ili kulinda usalama wake.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwasilisha ujumbe wa Tanzania kwa Wakuu wa Nchi na Serikali kwenye Mkutano wa ngazi ya juu wa Wakuu wa Nchi na Serikali 'Summit of the Future' uliofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Umoja wa Mataifa New York nchini Marekani jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# PM aomba UN kuunga mkono mataifa yasiyo uwezo kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema Umoja wa Mataifa hauna budi kuyaunga mkono mataifa madogo yasiyo na uwezo kiuchumi ili yaweze kuboresha mipango yao ya ndani.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akiwasilisha salamu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye ufunguzi wa mkutano wa siku mbili wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Kujadili Hatima ya Siku Zijazo (Summit of the Future), jijini New York, Marekani.

Waziri Mkuu ambaye yuko Marekani akimwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwenye Mkutano wa 79 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA79), amewaeleza wajumbe wa mkutano huo kuhusu jitihada za serikali kwenye masuala ya uchumi, ulinzi na mabadiliko ya tabianchi.

Akifafanua kuhusu suala la uchumi, Waziri Mkuu alisema: "Umoja wa Mataifa tunauomba uyaunge mkono mataifa ambayo hayana uwezo ili yaweze kuboresha mipango yao kiuchumi waliyonayo ndani ya nchi yao. Tanzania tumepanga kujenga kesho iliyobora kwa watu wetu kwa kuimarisha kilimo, uwekezaji, viwanda, madini na maliasili."

"Unapozungumzia ujenzi wa kesho iliyo bora kwa watu wako, huwezi kufanikiwa kama hakuna nchi iliyo salama; kwa hiyo ulinzi na usalama ni suala la muhimu na tumeihakikishia jumuiya ya kimataifa kwamba pamoja na ulinzi wa ndani bado ulinzi kwa nchi jirani nao pia wa muhimu," alisema.

Kuhusu suala la mabadiliko ya tabianchi, Waziri Mkuu alisema hivi sasa dunia inashuhudia athari kubwa kwenye baadhi ya nchi kutokana na shughuli za kijamii ikiwamo ukame, mvua nyingi zinazobababisha mafuriko. "Tanzania iko kwenye harakati za kuelimisha wananchi wake kuhusu mabadiliko ya tabianchi ili waweze kukaa pamoja na kujadiliana namna ya kukabiliana nayo huku wakiendelea na kazi zao za kiuchumi."

Aliwataka wajumbe wa mkutano huo wachukue hatua madhubuti za kupunguza uzalishaji wa hewa chafu, kulinda baioanwai na kuunga mkono jitihada za kukabiliana na hali hiyo katika nchi zinazoendelea. "Tanzania ina nia ya dhati ya kutetea masuala ya hali ya hewa duniani na inaitaka jumuiya ya kimataifa itimize ahadi zake za utoaji fedha za kusaidia masuala ya hali ya hewa na uhamishaji wa teknolojia."

Mapema, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Gutierres, alisema mkutano umeitishwa wakati huu ili waweze kutafuta mbinu za kuikomboa dunia kutoka huko inakoelekea na kuirejesha kwenye mstari wake. "Dunia imehama kwenye reli na sasa tunahitajika kufanya maamuzi magumu ili tuweze kuirejesha kwenye njia sahihi," alisema.

"Niliitisha kikao hiki kwa sababu changamoto za karne ya 21 zinahitaji kutatuliwa na majibu ya karne ya 21 kwa kupitia mifumo ambayo imeundwa vema, iliyo jumuishi na inayohitaji utaalamu wa watu wote."

Akiainisha changamoto hizo, Katibu Mkuu huyo alizitaja baadhi kuwa ni kukithiri kwa migogoro kuanzia Mashariki ya Mbali hadi Ukraine na Sudan huku kukiwa hakuna matumaini ya kuisha; mifumo ya usalama inayotishiwa na migawanyiko ya kijiografia, matishio ya kinyuklia na utengenezaji wa silaha mpya za kisasa na uwekezaji wa fedha kwenye uharibifu na vifo badala ya kuleta matumaini na fursa mpya.

Kaulimbiu ya mkutano wa mwaka huu ni "Hakuna kuachwa nyuma yeyote: Kushirikiana pamoja kuendeleza amani, maendeleo endelevu na heshima ya binadamu kwa vizazi vya sasa na vijavyo".

# Maonesho Siku ya Viwanda Vidogo yaiva

**Na Joseph Mwendapole**

CHAMA cha Wamiliki wa Viwanda Vidogo na Wazalishaji Wadogo Tanzania (TASSIM) kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, kimepanga kufanya maonesho ya Siku ya Viwanda Vidogo Tanzania (TAMISID) yatakayofanyika jijini Dodoma.

Maonesho hayo yatafanyika kuanzia Oktoba 28 hadi Novemba Mosi, mwaka huu, katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete lengo kuu likiwa kusherehekea mchango mkubwa wa viwanda vidogo katika kuboresha uchumi wa Tanzania.

Mwenyekiti wa TASSIM, Ali Masoud, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa Siku ya Viwanda Vidogo Vidogo jijini Dar es Salaam huku akisema tukio hilo muhimu linakusanya zaidi ya washiriki 1,000 wakiwamo wamiliki wa viwanda vidogo, wazalishaji, watunga sera, wataalamu wa sekta na wawakilishi kutoka sekta ya umma na binafsi.

Alisema takribani washiriki 500 wanatarajiwa kupata jukwaa la kipekee la kuonesha bidhaa na huduma za kibunifu, kukuza mtandao na kushiriki mijadala yenye maarifa kuhusu sekta hiyo.

Masoud alisema malengo ya Siku ya Viwanda Vidogo Tanzania yanalenga kuimarisha sauti za jamii ya viwanda vidogo, kutambua mchango na kusherehekea mchango mkubwa wa viwanda vidogo na wazalishaji wadogo katika maendeleo ya uchumi.

Alitaja malengo mengine kuwa ni kuweka mazingira yanayochochea ubunifu na ushindani ndani ya viwanda vidogo, kuongeza uelewa miongoni mwa makundi mbalimbali kuhusu nafasi ya viwanda vidogo katika uendelevu wa uchumi na maendeleo na kuonesha matunda ya viwanda vidogo kwenye uchumi.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, washiriki wataona bidhaa na huduma bunifu kutoka kwa zaidi ya wamiliki wa viwanda vidogo 500 na kwamba maonesho yatasaidia kuunganisha biashara na kuwezesha ushirikiano unaokuza fursa za ukuaji.

Pia alisema katika hafla hiyo, itatolewa elimu kuhusu viwanda, mwelekeo wa sekta, mbinu bora na mikakati ya kukabiliana na changamoto zinazokabili viwanda vidogo.

Alisema washiriki wataungana na wadau muhimu wa sekta ikiwamo taasisi za kifedha, watunga sera, wawakilishi wa mashirika ya kiraia na wasomi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. John Simbachawene, alisema serikali imewaalika wananchi na wadau mbalimbali kuhudhuria mkutano wa kukusanya maoni kuhusu Sera Mpya ya Biashara Ndogo Ndogo (SME) utakaofanyika mkoani Dodoma.

Alisema serikali ilikusanya maoni ya watu mbalimbali kwenye awamu ya kwanza hivyo imeamua kuandaa mkutano wa awamu ya pili kuchukua maoni kwa wale ambao walikosa nafasi kwenye awamu ya kwanza.

Mkutano huo, alisema utafanyika wiki hii mkoani Dodoma na kuwataka wananchi, wajasiriamali, wafanyabiashara kushiriki kwenye mkutano huo ili watoe maoni ya kuchangia kuboresha sera hiyo.

"Wizara inaendelea kuifanyia kazi sera mpya ya viwanda na tumeitisha mkutano wa wadau mbalimbali mkoani Dodoma waje kutoa maoni yao kwa awamu ya pili kwa ambao hawakutoa maoni yao ili tukamilishe hiyo sera na iweze kutoa mchango wake kwenye taifa letu na tuweze kuizindua rasmi," alisema.

Alisema lengo kuu la siku ya viwanda vidogo ni pamoja na kuongeza uelewa wa mchango wa viwanda vidogo katika uchumi na kukuza ubunifu kwenye sekta.

# Othman afichua chanzo cha uharibifu wa misitu

Na Mwandishi Wetu



MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema moja ya sababu za kuwapo uharibifu mkubwa wa misitu Zanzibar ni mifumo ya usimamizi inayotoa mwanya kwa baadhi ya watu kuingia na kujimilikisha na hatimaye kuuza maeneo ya serikali.

Othman aliyasema hayo jana katika kitongoji cha Kongole, Kijiji cha Bwejuu Wilaya ya Kusini Unguja alipotembelea maeneo yaliyoharibiwa ambayo yataingizwa katika mpango wa taifa wa kuirithisha Zanzibar kuwa ya kijani kwa kupandwa miti ya aina mbalimbali.

Othman alisema suala hilo ni miongoni mwa changamoto kubwa iliyoko Zanzibar katika maeneo mbalimbali ya hifadhi za ardhi na misitu ambayo yanahitaji kurekebishwa kwa kuondoa mifumo inayoruhusu watu kuingia, kuharibu na kujimilikisha ardhi na kuuza kwa watu mbalimbali.

Alisema serikali inaona uhai na maisha ya watu na mustakabali wa Zanzibar ni kuhakikisha Zanzibar inabaki kuwa ya kijani ndiyo maana ikafikiria kuanzisha na kuutekeleza mpango wa pamoja wa kitaifa wa kuirithisha Zanzibar kuwa ya kijani unaowahusisha watu na taasisi zote.

Alitanabaisha kwamba katika kutekeleza hilo, serikali inalazimika kuangalia sababu mbalimbali zinazochangia uharibifu wa mazingira hasa kwa maeneo yaliyotangazwa kwamba ni hifadhi hayawezi kumilikiwa mtu mwingine kwa kuwa na hati miliki.

Othman alisema kuna umuhimu mkubwa wa kurekebisha mifumo hiyo ili kuhakikisha inaimarishwa ili kuepusha masuala ya hifadhi kuharibiwa na watu kupitia mbinu hizo za uvamizi na kujimilikisha.

Alisema hivi sasa serikali kupitia wataalamu wake wa ndani, inaendelea kufanya tathmini juu ya mahitaji katika utekelezaji wa mpango wa kuirejesha Zanzibar kuwa ya kijani na kutafuta nyenzo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo kwa ufanisi zaidi.

Akiwa katika eneo la kitalu cha uatikaji wa miche ya miti ya misitu na matunda ya aina mbalimbali Kibele, alitaka Idara ya Misitu na Maliasili kufikiria kuwapatia miche kwa kuzingatia mahitaji ya kibiashara ili kupata fedha za kujiendesha.

Pia aliwataka wananchi na vikundi mbalimbali kuendelea kuhimizana na kushirikiana na vikundi mbalimbali pamoja na serikali katika kuhakikisha Zanzibar inakuwa ya kijani.

Mkuu wa Wilaya ya Kusini, Kassian Galosi Nyimbo, alisema serikali ya wilaya imekuwa na ushirikiano mkubwa na taasisi na wananchi katika kwa kupiga marufuku matumizi ya misitu iliyohifadhiwa ili kuhakikisha mazingira ya maeneo hayo hayaendelei kuharibiwa.

Alisema kutokana na jitihada za pamoja zinazoendelea kufanywa, wamewakamata watu mbalimbali wanaojihusisha na uharibifu wa misitu ikiwamo kukata miti na kuchoma mkaa. Alisema baadhi ya watu hao wamefikishwa mahakamani kutokana na tuhuma hizo.

Kutokana na ushirikiano huo, alisema hivi sasa serikali katika wilaya hiyo haiwezi kutoa kibali kwa watu walionunua ardhi kisirisiri na kuwaeleza wale walionunua ardhi katika mtindo wa aina hiyo kwamba ardhi iliyohifadhiwa haitumiki kwa mfumo huo isipokuwa kwa vibali maalum.

Naye Mjumbe wa Kamati ya Hifadhi ya Bwejuu, Mohammed Juma, alisema uvamizi na uharibifu wa ardhi ambayo ni maeneo ya akiba ya serikali katika eneo hilo bado ni changamoto kubwa licha ya kuwapo ushirikiano katika mamlaka mbalimbali kupambana na hali hiyo.


cotex industries

TAARIFA KWA UMMA



DEOCLES LUCAS MUJUNI

Hii ni kuutaarifu Umma kwamba mwenye picha hapo juu **DEOCLES LUCAS MUJUNI** Anatuhumiwa kuondoka na fedha za ofisi katika tawi alilokuwa anafanyia kazi mkoa wa Mwanza. Hivyo anatafutwa na mwajiri wake **COTEX INDUSTRIES LTD Mbezi Beach, Jogoo, Dar es salaam na Mwanza kuanzia tarehe 17/9/2024**

Tunaomba kuutangazia Umma kwamba Kampuni ya **COTEX INDUSTRIES LTD** haitahusika na miamala itakayoingizwa au shughuli yoyote itakayofanywa na mtajwa hapo juu kwa jina la Kampuni.

Tafadhali wasiliana nasi kwa **0657 801 444** kama una taarifa yoyote kuhusu Kupatikana kwake au toa taarifa Kituo cha Polisi **Igogo Mwanza** au kituo chochote cha polisi kilicho karibu yako.
**CASE NO IGO/RB/6516/2024 NA KUMBUKUMBU NA. IGO/IR/6829/2024**

**ZAWADI ITATOLEWA KWA ATAKAYE FANIKISHA UPATIKANAJI WAKE**

**Utawala.**


## Wazee walaani kubomolewa sanamu ya Nyerere

**NA Benny Kingson,** TABORA

WAZEE maarufu mkoani Tabora, wamelaani kitendo kilichofanywa na watu cha kuangusha sanamu ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, katika eneo la Taasisi mjini hapa, kisha kuivunja na kuchukua fimbo yake.

Wazee hao walilaani tukio hilo wakati Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha, alipotembelea kukagua marekebisho yanayoendelea kufanywa baada ya kuirejesha sanamu hiyo juu akiwa ameambatana nao pamoja na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wa serikali.

Chacha alisema ameamua kuwaita wazee hao ili kumpa mawazo ya nini kifanyike baada ya kutokea tukio hilo ambalo si la kawaida ndipo wazee hao walipotoa kauli kwamba kitendo hicho si cha kiungwana na waliohusika watapata matatizo katika maisha yao.

'Wazee hawa wamelaani watu wote wliohusika na watapata shida sana, vinginevyo waje kwangu waombe radhi hadharani ili niwaombee msamaha kwa wezee na kama wanadhani tunatania wasubiri waone kitakachowapata," alisema.

Alisema wamegundua kuwa tukio hilo halihusiani na mambo ya siasa bali ni masuala ya kijamii yanayolenga ushirikina kwa kutaka kujipatia umaarufu mkubwa kama alikuwa Hayati Mwalimu Nyerere na kwamba huko ni kujisumbua kwa kuwa hawatafanikiwa.

Chacha alisema watahakikisha wanaimarisha ulinzi na usalama na kuweka huduma ya umeme katika eneo hilo na kwamba kuna mpango wa kuboresha na kujenga majengo yote ili kuimarisha miundombinu kwenye eneo hilo la kihistoria.

'Tunaweka mambo sawa. Hapa pana historia kubwa sana ya ukombozi wa nchi na ni kielelezo na kumbukumbu muhimu pia ni eneo la kujifunzia kujua harakati za Mwalimu Nyerere zilifanyika hapa. Tutaweka utaratibu ili nyie wazee muwe mnatoa elimu kwa watu watakaokuwa wanafika hapa," alisema.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wazee Tabora, Harun Mbeyu, alisema wamekuwa wakisisitiza tangu awali kufanyika marekebisho katika eneo hilo ili kulipa hadhi na heshima inayostahili na kwamba walitoa tahadhari mapema kuhusu usalama wa sanamu hiyo kuwa uzingatiwe.

Mbeyu ambaye ni Meneja Mstaafu wa Kanda ya Magharibi wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), alisema walishauri uongozi wa manispaa, mkoa na CCM kuweka miundombinu inayostahili kwenye eneo hilo lenye sanamu ili kuleta tija na ufanisi zaidi lakini kumekuwa kunatolewa maagizo ambayo hayajatekelezwa.

'Unajua hapa ndipo eneo Mwalimu Nyerere alihutubia wananchi na kutokwa machozi akidai uhuru toka kwa wakoloni na palifanyika mkutano huo baada ya kupigwa kura tatu za uamuzi wa busara wa kumwondoa mkoloni, hivyo pana historia kubwa sana ya harakati za ukombozi wetu," alisema.

Diwani wa Mpera, Haruna Msoga, akiwa miongoni mwa wazee hao, alisema sanamu hiyo yenye kilo 600 aliileta kutoka Arusha mwaka 1988 kwa ajili ya sherehe za CCM kitaifa mkoani hapa na kwamba iliwekwa eneo hilo la juu kwa msaada wa winchi.

Msoga alisema sanamu hiyo iliwekwa eneo hilo la Taasisi zilizoko ofisi za Ofisa Mtendaji wa Kata ya Chemchem na kwamba watu waliofanya uharifu huo ambao ni wahujumu Uchumi, walidhani ina madini na waliangusha ili wajinufaishe au wakapate uongozi kwa njia za ushirikina.

Tukio hilo lilitokea usiku wa Septemba 20, mwaka huu, kwa sanamu hiyo iliangushwa na watu wasiojulikana na kusababisha kuvunjika vipande tatu, kichwa, kiwiliwili kuanzia shingoni hadi kiunoni na kuanzia kiunoni hadi miguuni na fimbo yake kuchukuliwa.

Miongoni mwa mambo yaliyoashiria kuwapo kwa masuala ya ushirikina na imani potofu ni kukutwa kichwa cha sanamu hiyo kimevingilishwa kwenye shuka jeupe kama sanda, kitamba cheusi, suruali na sarafu ya Sh. 200.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabadiliko utendaji TANESCO yawe mfano kwa taasisi zingine

**WANANCHI** katika maeneo mbalimbali nchini, kwa miaka mingi wamekuwa wakilalamikia utendaji usioridhisha wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO). Miongoni mwa malalamiko hayo ni pamoja na wateja kucheleweshewa kufungiwa umeme baada ya kuwasilisha maombi ya huduma hiyo.

Aidha, wananchi pia wamekuwa wakilalamikia watendaji wa shirika hilo kufika eneo la tukio inaporipotiwa kuwapo kwa jambo fulani kama vile hitilafu, kuharibika kwa transfoma na nyaya kuwa na matatizo kwa sababu ya kunguru kuzigonganisha. Baada ya kuripotiwa kwa tukio husika, wahusika walikuwa wakichelewa hadi wiki moja au zaidi kulishughuliki tatizo hilo.

Mbaya zaidi, baadhi ya watumishi hao hasa mafundi, baada ya kuripotiwa kwa tukio, wamekuwa wakiwadai wateja kuwapa chochote ili wawafanyie kazi zao kwa haraka au kuwauliza kama wana usafiri wa kuwapeleka na kuwarudishac eneo la tukio. Hiyo yote ilitasfiriwa kuwa ni mazingira ya watumishi hao kuwashawishi wateja kutoa rushwa.

Lakini katika maandiko matakatifu kuna msemo kwamba ya kale yamepita na sasa yamekuwa mapya. Hivyo ndivyo hali ilivyo sasa kwa TANESCO baada ya kufanya mageuzi makubwa ya kiutendaji. Hivi sasa huduma za shirika hilo zimeimarishwa kwa kiasi kikubwa na malalamiko yamepungua tofauti na ilivyokuwa zamani.

Hayo yamo katika hotuba ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Boteko, wakati akizungumza wiki iliyopita na wananchi wa Kigoma katika hafla ya uwekaji wa mawe ya msingi ya mradi wa umeme katika maporomoko ya Malagarasi ujenzi wa kituo cha kupokea, kupoza na kusambaza umeme katika eneo la Kidahwe.

Kwa mujibu wa Dk. Biteko, taarifa hiyo ya kuboreshwa kwa utendaji wa kazi TANESCO haikufanywa na shirika wala serikali bali taasisi inayoheshimika duniani kwamba hivi sasa mambo ndani ya taasisi hiyo ya umma ni mazuri. Kwa mantiki hiyo, shirika hilo limezaliwa upya kiutendaji na malalamiko yaliyokuwapo awali sasa ni historia.

Pamoja na kuwapo kwa mabadiliko hayo ya kiutendaji, Dk. Biteko alisema sifa hizo zinapaswa kuongezeka kwa shirika kupandisha zaidi viwango vya kiutendaji badala ya kubweteka na kurudia hali ya zamani kama msemo kwamba mgema akisifiwa tembo hulitia maji. Kwa mantiki hiyo, Naibu Waziri Mkuu Biteko alisema aliiambia menejimenti ya TANESCO kutolewa sifa hizo badala yake waendelee kuchapa kazi kwa viwango vya juu zaidi.

Kwa hakika, kupanda kwa viwango hivyo vya kiutendaji vilivyofanyiwa tathmini ya kimataifa, kumetokana na mipango na mikakati iliyowekwa na uongozi pamoja na Bodi ya Wakurugenzi ambayo inajumuisha wasomi nguli na wahandisi wabobezi katika sekta ya nishati pamoja na wataalamu wa masuala ya menejimenti. Kuwamo kwa wasomi hao wakiwamo waliowahi kuongoza taasisi nyeti na mabadiliko ya menejimenti yaliyofanyika karibuni, ni kielelezo kwamba hakuna mzaha katika utendaji.

Sifa linazopewa shirika hilo ambalo lina dhamana kubwa ya kuwapatia umeme kupitia kauli mbiu ya 'Tunaayangazia Maisha Yako', zinapaswa kuwa kigezo kwa taasisi zingine za umma zilizopewa majukumu ya kuwapatia wananchi huduma bora zikiwamo maji.

Katika kufanya kazi na kupata sifa za kiwango cha kimataifa, hakuna miujiza bali ni kufanya kazi kwa bidii na maarifa ikiwamo kuweka mikakati endelevu katika kufikia malengo yaliyowekwa.

Kwa suala la umeme, kwa mfano, kulikuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa suala hilo lakini sasa umefika mpaka vijijini na umewasaidia vijana kujiajiri kwa kutengeneza vitu mbalimbali. Pia katika baadhi ya maeneo TANESCO ilikuwa ikitumia majenereta kuzalisha nishati hiyo lakini sasa yameanza kuondolewa baada ya kusambazwa kwa umeme wa gridi ya taifa katika mikoa ya pembezoni kama Rukwa, Katavi, Kigoma na Kagera.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Watoto wanatamani elimu, wasaidiwe

**KATI** ya Julai 2021 hadi Aprili mwaka huu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Jinsia na Makundi Maalum, imewaunganisha watoto 1,346 na familia zao.

Watoto hao ni miongoni mwa 6,459 ambao wizara hiyo iliwabaini wakati wa kutambua watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani, ambapo pia 816 kati ya hao wakiunganishwa na mafunzo ya stadi za maisha.

Hayo ni kwa mujibu wa Waziri wa wizara hiyo, Dk. Dorothy Gwajima, akifafanua kuwa maeneo yenye watoto wengi ni Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Mwanza, Dodoma na Iringa.

Pamoja na jitihada hizo, bado katika maeneo ya mijini, imekuwa ni jambo la kawaida kukuta watoto wenye umri wa kwenda shule, wakiomba msaada wa fedha na wengine wakiuza vitu vidogo kama karanga, pipi, biskuti na vitu vingine kadhaa.

Zipo sababu mbalimbali zinazotajwa kuchangia uwapo wa watoto hao mitaa, ambao kama hakutakuwa na juhudi za makusudi za kuwanusuru, taifa linaweza kuwa watu wazima wa baadaye wasio na msaada.

Miongoni mwa sababu hizo ni kutengana kwa wazazi wao au wote kufariki dunia, hivyo kuwalazimisha kutafuta maisha kwa kuomba msaada wa fedha au kufanya biashara ndogo ili kujipatia kipato.

Inasikitisha kuona watoto wa umri wa kuwa shuleni, lakini badala yake wanakaa mitaani bila kupata elimu, ambayo huenda baadhi wangekuwa wataaalamu wa fani mbalimbali wa baadaye kama wangesoma.

Ninadhani ni vyema kuwa kuwapo kwa hatua madhubuti za kukabiliana na mazingira hayo, ili kunusuru kizazi kijacho ili kiwe na faida kwa taifa lao, kwa kutambua kuwa vijana ni taifa la kesho.

Mojawapo ya hatua ambazo zinapaswa kuchukuliwa, ni wazazi na walezi kuzingatia malezi bora na kuepuka mifarakano ili kuwafanya watoto watulie nyumbani badala ya kukimbilia mitaani.

Wadau wote wakiwamo wa ustawi wa jamii, waendelee kuelimisha umma umuhimu wa malezi bora, ili kusaidia watoto wenye umri kutulia nyumbani na kwenda shule, wasome badala ya kurandaranda mitaani wakiomba msaada au kufanya biashara ndogo, kwa sababu ya changamoto za wazazi wao.

Lakini pia serikali ipige marufuku watoto na vijana wenye umri wa kwenda shule kurandaranda mitaani au kufanya biashara kwenye vituo vya mabasi. Kitendo ambacho kinachangia kuwafanya wakose elimu.

Marufuku iwe ni ya kudumu na iende sambamba na mikakati ya kuwawezesha kupata elimu, badala ya kuwaondoa leo, lakini baada ya siku chache wanarudi tena mitaani kuendelea kuomba.

Imekuwa ni jambo la kawaida kwa miaka mingi kuona wakiondolewa mitaani lakini baada ya siku chache huwa wanarudi. Kitendo ambacho kinaonyesha kuwa huenda hakuna hatua madhubuti.

Si vibaya wakaondolewa na kupelekwa vituo maalum vyenye shule chini ya uangalizi, ili waweze kupata elimu, kwani katika kundi hilo, inawezekana wapo wenye vipaji lakini hawajapata fursa.

Vilevile, jambo la msingi ni kuimarisha idara zinazohusiana na masuala ya elimu ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto. kisha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, ambayo moja ya majukumu yake ni kuratibu na kuitafutia majibu changamoto hiyo, ifanye kazi yake.

Wanaweza kuwachukuliwa na kuwapeleka kwenye vituo vya serikali ya kulelea watoto wenye mahitaji maalum hasa wenye kuhitaji shule, kwani elimu ni muhimu kwa mtoto, hivyo, anapaswa kuipata.

Ingawa kuwaita watoto wa mitaani kunapingwa kwa maelezo kuwa mitaa haizai watoto, ninakosa jina la kuwaita. Lakini hata liwe jina gani jambo la msingi ni kuwatoa katika mazingira hayo.

## Naibu Waziri ainyoshea kidole TAKUKURU

**Na Lusungu Helela,** TABORA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu ameitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwa mfano kwa kujipambanua kutenda haki na kuonesha uadilifu katika jamii.

Pia amesisitiza hatua kali kuchukuliwa dhidi ya mtumishi yeyote wa TAKUKURU atakayebainika kutokuwa mwadilifu.

Sangu ametoa kauli hiyo jana baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa ofisi za TAKUKURU Wilaya ya Nzega mkoani Tabora uliogharimu Sh. milioni 314.2 hadi kukamilika.

Alisema TAKUKURU ni chombo kinachohitaji watumishi wenye uadilifu wa hali ya juu, hivyo kwa mtumishi yeyote ambaye si mwadilifu, TAKUKURU si mahali sahihi kwake kufanya kazi.

Naibu Waziri Sangu alisema ni jambo lisilokubalika kwa chombo hicho nyeti cha kuzuia rushwa kuwa na watumishi mabingwa wa kupokea rushwa.

Kuhusu ujenzi wa ofisi hizo, Sangu aliipongeza TAKUKURU kwa kuonesha mfano namna fedha za Watanzania zinavyotakiwa kutumika kwa kuwa thamani ya fedha iliyotumika kwenye ujenzi wa ofisi hizo inaonekana.

"TAKUKURU ni chombo kinachosimamia uadilifu na kinatakiwa kiwe cha kwanza kuonesha uadilifu kwa matendo yake. Kwa namna nilivyokagua jengo hili, nimeridhishwa mno na naamini wateja watakaokuja hapa kwa ajili ya kuchunguzwa, hili jengo litumike kama mfano kwa kuonesha thamani ya fedha iliyotumika. Niwapongeze sana kwa jambo kubwa mlilolifanya hapa," alisisitiza Sangu.

Sangu pia aliiagiza TAKUKURU kuhakikisha inahamia katika ofisi hizo za kisasa ndani ya mwezi huu, kwa kuwa ofisi inazozitumia kwa sasa, kodi ya pango itafikia ukomo mwezi huu.

Alisema kukamilika kwa ofisi hizo kunaonesha dhamira ya dhati ya serikali katika kuhakikisha TAKUKURU inawajibika ipasavyo kwa wananchi.

Sangu alitumia fursa hiyo kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa maono yake makubwa ya kukubali kutoa fedha hizo ili kuhakikisha watumishi wa TAKUKURU katika wilaya ya Nzega wanatimiza wajibu wao kwa kufanya kazi katika ofisi za kisasa.

Katika hatua nyingine, Sangu alitaka TAKUKURU kuzifanyia kazi kwa wakati nyaraka za mikataba ya miradi ya maendeleo ambazo huwasilishwa kwao kutoka kwa wateja wao.

Amesema kama jambo limekamilika au halina uchunguzi wowote ni muhimu nyaraka hizo zikarudishwa haraka kwa wahusika badala ya kukaa nazo kwa muda mrefu kwa kuwa lengo la TAKUKURU kupewa nyaraka hizo ni kuzuia rushwa ili kuhakikisha miradi ya maendeleo inapoanza kutekelezwa isiharibike.

Alisisitiza kuwa ni muhimu kwa nyaraka hizo za mikataba kufanyiwa kazi ipasanyo ili kuhakikisha miradi hiyo ya maendeleo inakamilika kwa viwango vinavyotakiwa kwa kuonesha thamani ya fedha.




Mkurugenzi wa Sheria wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake katika Usafiri wa Anga Tanzania, Maria Memba, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kuzindua shindano la ubunifu wa nembo ya jukwaa hilo kwa wasichana wenye umri kati ya miaka 14 hadi 20 nchini, pamoja na mkutano wa wanawake viongozi wanaohudumu katika sekta ya usafiri wa anga, unaotarajiwa Oktoba 31 jijini Dar es Salaam. **PICHA: DICKSON MULASHANI**

# SMZ kujenga hospitali kubwa ya mkoa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema itajenga hospitali kubwa ya mkoa maeneo ya Mahonda, Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa ufadhili wa serikali ya Oman.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar alipokutana na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Oman anayeshughulikia Utawala na Fedha, Khalid Almuslahi.

Dk. Mwinyi alisema ujenzi wa hospitali hiyo ni muhimu kwa dhamira ya serikali ya kuwa na hospitali kubwa kwa kila mkoa ili kuwafikishia wananchi huduma bora karibu na makazi yao na kupunguza msongamano kwenye Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano, Ikulu, Zanzibar, Dk. Mwinyi aliipongeza serikali ya Oman kwa kushiriki kikamilifu kwenye miradi ya maendeleo visiwani humo kwa taasisi mbalimbali za nchi hiyo kuiunga mkono Zanzibar kiufundi na kitaalamu.

Dk. Mwinyi alimhakikishia Naibu Waziri huyo kwamba uhusiano uliopo baina ya Zanzibar na Oman ni imara, hivyo miradi ya ushirikiano inayoendelea itawekwa mkazo zaidi katika kudumisha uhusiano wa diplomasia baina ya pande mbili hizo.



**Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar alipokutana na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Oman anayeshughulikia Utawala na Fedha, Khalid Almuslahi.**

Kuhusu Mji Mkongwe wa Zanzibar, alisema ni eneo muhimu la urithi linalohitaji kuendelezwa wakati wote, hivyo juhudi zinazofanywa na Serikali ya Oman ya kuukarabati na kuuimarisha ni kuunga mkono juhudi za SMZ kuinua uchumi wa nchi.

Alisema Mji Mkongwe mbali na kuwa kivutio cha utalii, pia ni eneo muhimu la kukuza uchumi na utamaduni wa Zanzibar na serikali itaendelea kuchukua juhudi mbalimbali za kuutunza mji huo.

Serikali ya Oman katika kuendeleza ushirikiano wake na Zanzibar, inafadhili miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa hospitali, ukarabati wa Mji Mkongwe, huduma za maji, umeme na elimu.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Bashe aagiza mwongozo bei mbolea

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, ameiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), kutoa mwongozo wa bei za jumla na rejareja kwenye kila kituo kinachouza pembejeo nchini.

Bashe alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea maghala mbalimbali ya uhifadhi na uuzaji wa mbolea mjini Songea.

Pia alitembelea ghala la Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) lililokarabatiwa kwa ajili ya kuhifadhi na kuuza mbolea za kupandia aina ya DAP na za kukuzia aina ya UREA katika eneo la viwanda la Ruhuwiko, mjini humo.

"Ghala hili lina ukubwa wa mita za mraba 5,000 kwenye ekari 16 na lina uwezo wa kuhifadhi tani 20,000 za mbolea na litatoa huduma katika mkoa wa Ruvuma na wilaya zake zote," alisema.

Aidha, kwa nyakati tofauti, Bashe alizungumza na wafanyabiashara kujadiliana nao mambo mbalimbali zikiwamo bei wanatoza kwa wakulima.

"Nashauri mkae pamoja kuwa na uwiano wa bei ambayo haimwumizi mkulima na pia iwe bei yenye gharama za uhalisia," alisema.

Kuhusu viuatilifu, Waziri Bashe aliielekeza Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) kuhakikisha viuatilifu vinasambazwa nchini na kuimarisha mfumo wa kanzidata kuongeza taarifa ya muuzaji na mnunuzi na kuweka msimbomilia (QR Code) kwenye kila chupa au bidhaa.

Wafanyabiashara hao waliokutana na Bashe wanatoka mkoa wa Ruvuma wanajishughulisha na uuzaji wa mbolea na mazao mbalimbali yakiwamo mahindi.

Waziri Bashe aliwaomba wafanyabiashara hao endapo watakuwa tayari, wajenge maghala ndani ya Mkoa wa Ruvuma na kwamba wizara itaingia nao mikataba kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ili kukodi kwa ajili ya kuhifadhi nafaka hadi za miaka 10.



Mjumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Dk. Zakia Mohamed Abubakar (kulia), akiangalia mafunzo kwa vitendo yaliyokuwa yakifanywa na waandishi wasaidizi na waendesha vifaa vya bayometriki (BVR), alipotembelea mafunzo hayo jana, katika Shule ya Sekondari Mwanamwema Shein iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini mkoani Singida. Mkoa wa Singida na Dodoma wanatarajia kuanza uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura Septemba 25 hadi Oktoba mosi, mwaka huu. **PICHA: INEC**

# Wananchi kupewa elimu fursa biashara hewa ukaa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WANANCHI wa Wilaya ya Gairo, mkoani Morogoro wanatarajiwa kupatiwa elimu ya matumizi ya nishati safi kwa ajili ya kulinda mazingira na afya ili kuchangamkia fursa ya biashara ya hewa ukaa.

Mkuu wa wilaya hiyo, Jabir Makame, alisema hayo wakati akielezea maandalizi ya maonesho makubwa ya kilimo biashara yaliyopewa jina la Samia Kilimo Biashara Expo 2024, msimu wa tatu.

Alisema maonesho hayo yamepangwa kufanyika Oktoba 6 hadi 12, mwaka huu na yatawakutanisha wananchi na wakulima pamoja na wadau wanaohusika katika mnyororo wa thamani wa sekta ya kilimo, mifugo na mazingira.

"Tumetenga siku maalumu ambayo itakutanisha wadau na wananchi kujadiliana kuhusu matumizi ya nishati safi na fursa ya biashara ya kaboni," alisema Makame.

Alisema kuwa Gairo inatekeleza kampeni ya urithi wa kijani yenye lengo la kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, akielezea matumizi ya nishati safi ya kupikia, alisema mkoa unaendelea kusimamia ajenda kuu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa kinara wa Afrika na Dunia kwenye masuala ya nishati safi ya kupikia.

"Sisi kama mkoa tumeichukulia kwa nguvu kabisa ajenda hii, mfano Wilaya ya Ulanga kuna uzalishaji wa mkaa mbadala ambao unazalishwa kwa kutumia mabaki ya mbao na pumba za mpunga," alisema Malima.

Alisema kwa Manispaa ya Morogoro kipo kiwanda cha mwekezaji kinachozalisha mkaa mbadala kwa kutumia majani ya kupandwa.

"Zipo aina nyingi za fursa, maonesho makubwa haya ya Gairo yatatumia pia kuonesha uwezo mkubwa wa uoneshaji wa nishati mbadala kwa watumiaji wa mkaa hasa kwenye maeneo haya ya miji ili wabadilike," alisema Malima.

Alisema ili kuwezesha matumizi ya nishati mbadala kuwa endelevu, kuna haja ya kujipanga kuweka tozo kubwa ya kuingiza mkaa unaotokana na miti ili kudhibiti misitu isiendelee kuharibiwa.

"Utaratibu wa kutumia nishati safi ya kupikia ni njia salama kwa afya hasa kwa wanawake na wadau wengine wanaojishughulisha na upikaji," alisema Malima.

Pia alisema uhusiano wa mazingira, uchumi, kilimo na maisha ya kila siku ya binadamu ni jambo kubwa zaidi.

# Watalii kufikia mil. 5 mwakani

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imesema itaendelea kuweka nguvu na kuimarisha sekta ya utalii ili kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni tano ifikapo mwaka 2025.

Uamuzi huo wa serikali unatokana na sekta hiyo kwa sasa kuchangia pato la taifa kwa asilimia 17 huku ikileta mafanikio kupitia hifadhi za taifa ikiwamo ya Mikumi iliyoko Mkoani Morogoro iliyofikisha miaka 60 tangu kuanzishwa.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, alisema sehemu ya mafanikio hayo yamechangiwa na jitihada zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia filamu maarufu ya "The Royal Tour" na ile ya "The Amazing Tanzania".

Alisema serikali inajivunia ongezeko kubwa la wageni wanaoendelea kutembelea kwenye hifadhi za taifa nchini na kuongeza chachu ya kukuza utalii wa ndani na nje ya nchi huku nchi ikiendelea kunufaika na mapato kutokana na wageni hao.

"Tunapozungumzia mafanikio ya utalii nchini hatuwezi kuacha kumtaja Rais Samia Suluhu Hassan kwani amefanya jitihada kubwa kujitoa kuzitangaza hifadhi zetu kupitia ile filamu The Royal Tour," alisema.

Katika mwaka 2023/24, alisema kutokana na filamu hiyo, idadi ya watalii wa kimataifa waliofika nchini imeongezeka kwa asilimia 96 kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi 1,808,205 mwaka 2023 na kuongeza kasi ya mapato kupitia sekta hiyo ya utalii.

Alisema kwa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi katika kipindi cha 2023/24, watalii 138,844 walitembelea hifadhi hiyo sawa na ongezeko la asilimia 198.48 kutoka watalii 46,517 waliotembelea hifadhi hiyo kwa mwaka 2020/21.

Kwa mujibu wa Waziri, ongezeko hilo linatokana na serikali kuendelea kuimarisha huduma kwa watalii kwa kuboresha miundombinu ya utalii ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na ujenzi wa barabara kurahisisha watalii kufikia vivutio mbalimbali.

Akitolea mfano wa maboresho makubwa ya miundombinu ya utalii ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, serikali kupitia mradi wa REGROW, inaboresha uwanja wa ndege kuwa wa kisasa katika eneo la Kikoboga, ujenzi wa malango ya watalii maeneo ya la Doma na Kikwaraza, ujenzi wa kituo cha kutoa taarifa kwa wageni (VIC), kambi za kupumzikia wageni, maeneo ya malazi na kuunganisha hifadhi kwenye gridi ya taifa.

Alisema miradi hiyo itakapokamilika itawezesha kuongeza idadi ya watalii kwa kuwa ndege kubwa zaidi zitaweza kutua ndani ya Hifadhi ya Taifa Mikumi na kwamba kwa wakati mmoja zaidi ya wageni 140 watahudumiwa kwa pamoja.

Naye Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Musa Kuji, alisema Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ilikuwa ikishika nafasi ya 14 kati ya 21 katika ukusanyaji wa mapato lakini sasa inashika nafasi ya sita kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu.





# 'Utulivu wananchi Ngorongoro wamkosha Samia'

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

MSHAURI wa Rais katika masuala ya siasa na uhusiano wa jamii, Balozi Rajab Luhwavi, amesema Rais Samia Suluhu Hassan anafurahishwa na utulivu wanaouonyesha wananchi wa Ngorongoro mkoani Arusha, baada ya serikali kuweka bayana umuhimu wa shughuli za uhifadhi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Akizungumza jana katika ibada ya shukrani iliyofanyika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Luka, lililoko katika Kata ya Endulen, wilayani hapa, Balozi Luhwavi, alisema kutokana na utulivu huo, Rais Samia ameelekeza wasaidizi wake kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa maelekezo yake yote katika eneo hilo.

"Serikali inawapongeza wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro, kwa kuendelea kudumisha umoja, amani na utulivu katika eneo hili, na hivyo kuendeleza falsafa ya R4 ya Rais, Samia Suluhu Hassan ya kutaka wananchi wote kuishi kwa maelewano na maridhiano," alisema.

Alisema falsafa ya Rais Samia ya 4R, inamaanisha Reconciliation (maridhiano au upatanisho), Resilence (ustahimilivu), Reforms (mageuzi au mabadiliko) na Rebuilding (kujenga upya).

Hivyo, aliwataka wananchi wa Endulen na Ngorongoro kwa ujumla, kuendelea kuwa wavumilivu wakati serikali katika ngazi mbalimbali ikiendelea kutekeleza maelekezo ya Rais Samia.

Kadhalika, alisisitiza umuhimu wa wananchi hao kuendelea kupendana na kushirikiana na serikali katika shughuli mbalimbali za maendeleo.

Hadi kufikia Agosti mwaka huu, takribani kaya 1,598 zenye watu 9,618 na mifugo 39,779 ilikuwa imehama kwa hiari ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro kupisha shughuli za uhifadhi ili kurejesha ikolojia yake baada ya makazi ya watu na mifugo kutishia uhai wa hifadhi hiyo.

Katika ibada hiyo, pia Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Dk. Elirehema Doriye, aliwaeleza wananchi hao kuwa mamlaka yake itasimamia na kutekeleza maelekezo yote yanayoihusu mamlaka hiyo yaliyotolewa na wawakilishi wa Rais Samia.

"Tayari hatua mbalimbali zimechukuliwa katika kutekeleza maelekezo hayo, ikiwa na pamoja na kuendeleza uhusiano wa NCAA na wananchi wa Ngorongoro," alisema Dk. Doriye.

Mbunge wa Ngorongoro, Emmanuel Ole Shangai, alipongeza serikali kwa kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha miradi mbalimbali ya maendeleo inatekelezwa, huku akisisitiza kuwa ataendelea kusimamia suala hilo ili kuleta maendeleo kwa wakazi wa eneo hilo.

# Tanzania yashika namba 5 idadi kubwa ya faru weusi

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

TANZANIA inashika nafasi ya tano Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya aina ya faru weusi.

Mtafiti wa faru kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Dk. Victor Kakengi, alisema hayo jana, kwamba duniani kuna aina tano za faru, ambazo zinapatikana kwenye mabara mawili pekee ambayo ni Afrika na Asia.

Alisema kanzidata ya faru iliyopo Wizara ya Maliasili na Utalii, inaonyesha kuwa Tanzania ina faru weusi 263.

"Katika Bara la Afrika, kuna aina mbili za faru, ambazo ni faru mweupe na faru mweusi, na kwa upande wa Bara la Asia, kuna spishi tatu za faru, ambazo ni Java, Sumatran na One horned rhino.

"Tofauti kati ya faru mweupe na faru mweusi, ambao wote wana rangi ya kijivu, ni kwamba faru mweupe anakula nyasi, umbile lake ni kubwa, mdomo wake una umbo la boksi na wanapenda kuishi pamoja.

...Tofauti na faru weusi, ambao wanakula majani na vichaka, wana mdomo kama ndoano au uliochongoka, wanapenda kuishi mmoja mmoja, wanaishi kwenye vichaka, na kwa umbile ni mdogo kuliko faru mweupe," alisema.

Alisema faru weusi wako kwenye orodha ya walio hatarini kutoweka duniani, huku Tanzania kupitia mpango wa taifa wa miaka mitano wa uhifadhi wa faru hao imeendelea kuwatunza 100 waliokuwapo tangu mwaka 1990 ambao sasa wamefikia 238.

Alisema hadi kufikia mwaka 2023, Tanzania ilikuwa na utajiri mkubwa wa faru, hasa katika Hifadhi za Taifa za Burigi/Chato, Serengeti na Mkomazi.



Mdau wa maendeleo Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Lazaro Leskar Ole Suya (katikati), akimkabidhi cheti cha kuhitimu elimu ya msingi mhitimu wa darasa la saba wa Shule ya Msingi New Light ya mji mdogo wa Mirerani, Andrew Lyimo, kwenye mahafali ya 13 ya shule hiyo juzi, kulia ni Mkurugenzi wa shule hiyo, Askofu Sommy Severua. **PICHA: GIFT THADEY**

# Maofisa ustawi jamii wawasilisha mapendekezo 13 kwa Gwajima

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MAOFISA ustawi wa jamii nchini wamewasilisha mapendekezo 13 kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima.

Mojawapo ya pendekezo ni hoja ya kuitaka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuruhusu kutungwa kwa sheria ndogo kila wilaya ya kudhibiti wazazi wanaowatumia watoto wadogo kuomba fedha mijini ili wajipatie kipato.

Mapendekezo hayo yaliyowasilishwa na Kamishna wa Ustawi wa Jamii nchini, Dk. Nandelwa Mhando, yanasadifu uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kutoa maelekezo ya kusukwa kwa idara ya ustawi wa jamii ili kuanza kujitegemea.

Kamishna Dk. Mhando, aliwasilisha mapendekezo hayo, katika mkutano wa tatu wa mwaka wa maofisa ustawi wa jamii uliofanyika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

"Kufanya ukaguzi na usajili wa watu wenye ulemavu ili kuwezesha utoaji wa huduma sahihi kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

Kila mkoa kuwasilisha takwimu za watoto wanaoishi mitaani ili waweze kuunganishwa na familia zao kwa asilimia 50 na zaidi na Wizara ya Fedha kuainisha mwongozo wa Bajeti wa Mwaka 2025/26 kwa kuweka afua ya ustawi wa jamii kama zilivyoainishwa afua zingine na kuweka mgawo wa 73 ya bajeti na kutekelezwa kama ilivyoainishwa katika mwongozo wetu," alisema.

Aidha, Kamishna Dk. Mhando, alitaja azimio lingine ni ofisi za mikoa na halmashauri zihakikishe zinatenga ofisi za ustawi wa jamii zenye vyumba vya kutosha vya kutoa huduma kwa kuzingatia faragha na siri za wateja pamoja na kujenga ofisi hizo kwa kuzingatia dhamana itakayotolewa na wizara.

Alisema wanataka pia, halmashauri zote nchini kwa kushirikiana na wadau, kuanzisha huduma za nyumba salama kwa ajili ya kuhifadhi waathirika wa ukatili.

"Kila halmashauri iandae mapendekezo ya utoaji wa elimu kwa umma na huduma ya M-KOBA kwenye jamii na kutoa taarifa kila robo mwaka kwenye mamlaka husika na mkutano wa mwaka wa maofisa ustawi wa jamii.

Alisema katika mkutano huo, maofisa hao wamependekeza kila halmashauri, ihakikishe inaratibu wadau wote wa serikali na sekta binafsi kwenye eneo lao na kuendesha vikao vya kupanga bajeti na ufuatiliaji wa huduma za ustawi wa jamii kila robo mwaka.

Vilevile, kila Halmashauri ilalizie ujengaji wa mifumo ya kielektroniki ya usajili wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na kuunganisha maadhimisho yote ya wenye ulemavu na wazee ili kuwapo na adhimisho moja kwa mwaka kwa kila kundi.

Liko pia la kufanya utambuzi wa ukubwa wa tatizo la kutoa huduma za waathirika wa matatizo ya afya ya akili, ili kupunguza tatizo kwa asilimia 20.

Kutokana na yote hayo, pia wanataka wizara hiyo iandae kikao cha makatibu wakuu wa wizara za kisekta ili kujadili namna bora ya kuboresha huduma za ustawi wa jamii.





# Wizi wa watoto, ubakaji watajwa kukithiri Geita

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Geita, Safia Jongo, amesema matukio ya wizi wa watoto yameongezeka mkoani Geita sambamba na vitendo vya ubakaji, huku mauaji yakishuka kutoka 89 kwa mwaka hadi 59.

Alibainisha hayo juzi wakati wa uzinduzi wa kampeni ya waambie kabla hawajaharibiwa iliyozinduliwa na Jeshi la Polisi Kitengo cha Dawati la Ukatili wa Jinsia mkoani hapa.

Jongo alisema matukio ya ubakaji yalikuwa 71 kwa mwaka jana lakini hadi kufikia Agosti mwaka huu matukio hayo yamefikia 91 na kwamba bado kuna tatizo la watoto kuibiwa hali inayotokana na wazazi kuwatelekeza watoto wao.

Alisema kampeni hiyo inalenga kuwafikia wanafunzi wa shule za msingi na sekondari pamoja na kuwalinda na kukomesha rushwa ya ngono, usagaji na watoto kujihusisha na ugaidi.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela alisema matukio ya ukatili mkoani humo bado ni tatizo ambapo kwa kipindi cha mwaka jana yalikuwa zaidi ya 209.

Aidha, alisema viongozi wa ngazi zote mkoani hapa wanaunga mkono Jeshi la Polisi katika kampeni hiyo ili kukomesha ukatili wa kijinsia hasa kwa watoto.

Shigela alisema kuwa wazazi, walezi wanao wajibu wa kutathmini kuhusu malezi ya watoto na kukomesha ukatili wa watoto sambamba na kuziacha mila na desturi zinazosababisha ukatili kwa watoto.

Mchungaji wa Kanisa la Wadiventisa Wasabato Kanisa la Mjini Geita, Joram John alisema kama wazazi na walezi hawataweza kuwalinda watoto taifa haliwezi kuwa na jamii yenye maendeleo.

# Aomba msaada mil.7/- kujiokoa asipate upofu

**Na Vitus Audax**

MKAZI wa Kisuke wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Ester Matanga (25) anayedaiwa kutobolewa macho na mtalaka wake Paulo Shija (19) Mkazi wa Kata ya Ndala Manispaa ya Shinyanga, yupo hatarini kupata upofu baada ya kukosa fedha kwa ajili ya matibabu katika Hospitali ya Rufani Kanda KCMC.

Kwa mujibu wa Ester matibabu hayo yanagharimu zaidi ya Sh. milioni saba ambako anadai yeye pamoja na familia yake hawana uwezo wa kupata fedha hizo, hivyo kuwaomba Watanzania kumchangia ili apate huduma hiyo.

Kwa mujibu wa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Kolandoto aliyempokea mgonjwa huyo kwa mara ya kwanza na kuanza kumpatia matibabu, Dk. Wallace Sahani alisema, Ester ametobolewa macho yote ila jicho mmoja limeharibika na lingine linahitaji matibabu ya kibingwa.

Dk. Sahani alisema matibabu hayo ya kibingwa anatakiwa kuyapata katika Hospitali ya Rufani Kanda ya KCMC ambako walimpa rufani kwenda baada ya kupata matibabu ya awali. "Jicho lake moja halioni vizuri kuna damu imevujia ndani hivyo tunalazimika kumpatia rufani akapate matibabu ya kibingwa ili aweze kuona vizuri, kwani alifika akiwa na hali mbaya akiwa na majeraha makubwa lakini kwa sasa tumeyaweka sawa," alisema Dk. Sahani.

Akizungumza nyumbani kwao juzi, Ester alisema ameshindwa kupata huduma za matibabu kwa kukosa Sh. milioni saba kwa ajili ya kufanyiwa upasuaji katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC.

Alisema awali alipatiwa matibabu katika Hospitali Teule ya Kolandoto na kupewa rufani kwenda KCMC, lakini mpaka sasa amesalia nyumbani bila msaada huku akihofia kupata ulemavu wa kudumu.

"Bado nina maumivu makubwa yaani macho yote bado yanauma na mishipa inauma naomba msaada angalau tu nipate kuona na kurejea katika hali yangu ya kawaida maana nikiona nitaweza kufanya hata kazi," alisema Ester.

Aidha alisema kwa sasa hali yake ni ya kuhudumiwa muda wote ikiwa ni pamoja na kupelekwa chooni kama mtoto, hivyo kuomba msaada ili akapate matibabu kupitia M-PESA 0768827164 Jina Lucia Juma Makaranga.





Madereva wa bodaboda wakivuka barabara eneo la Kivulini, Dar es Salaam jana, bila kusubiri kuruhusiwa na taa, kitendo ambacho kinaweza kusababisha ajali. **PICHA: SABATO KASIKA**

# EIB kusaidia upatikanaji maji Jiji la Mwanza

**Na Vitus Audax,** MWANZA

UJUMBE wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), umeanza kufanya upembuzi wa kukidhi vigezo vya kutoa fedha kwa Serikali ya Tanzania kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mwanza (MWAUWASA).

Fedha hizo ni kwa ajili ya mradi wa awamu ya pili wa usambazaji maji, mkoani hapa.

Akizungumza juzi mkoani hapa walipofika kufanya mazungumzo kuhusu mradi huo, Ofisa Mikopo wa EIB kwa Ukanda wa Afrika, Lily Munyigi alisema wanatarajia kuanza mradi huo mara moja baada ya taratibu zote kukamilika.

Alisema wana furaha kufanya kazi na Serikali ya Tanzania pamoja na ushirikiano mkubwa uliopo baina ya pande hizo mbili na kwamba jumuiya hiyo inajivunia amani iliyopo nchini kwani inaruhusu uwekezaji.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda alisema ushirikiano katika sekta hiyo muhimu umekuja katika wakati muafaka baada ya kukamilika kwa chanzo cha maji Butimba.

Alisema, baada ya chanzo cha maji Capripoint kuanza kuzidiwa kutokana na ongezeko la watu na kusababisha kero ya maji mkoani hapa, serikali ilianza utekelezaji wa mradi wa chanzo kipya cha Butimba ambacho tayari kimekamilika.

Alisema kukamilika kwa chanzo hicho kunahitaji zaidi uwekezaji huo ili kufikisha huduma hiyo muhimu kwa wananchi walioikosa kwa muda mrefu.

"Mwanza ina watu zaidi ya milioni tatu na hasa mjini ndiyo kuna ongezeko kubwa zaidi, tukiwa na maji ya kutosha na usambazaji wa uhakika tutakua na uhakika wa afya bora kwa jamii na kuongeza thamani ya uchumi wa mkoa kupitia shughuli za uzalishaji," alisema Mtanda.

Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Nelly Msuya, alisema hatua ya pili na ya tatu kwa mradi huo itaimarisha upatikanaji wa maji kwa kusambaza mtandao kwa kilomita 700 kwenye wilaya za Ilemela, Nyamagana, Magu na Misungwi.

Alisema baadhi ya maeneo mkoani Mwanza bado yanapata maji kwa mgawo, huku maeneo mengine yakikosa huduma hiyo, akisema mradi huo wa usambasaji wa maji unatarajiwa kusaidia kupunguza au kumaliza kabisa tatizo hilo.



Ukurasa 12

**Kwa kutumia TEHAMA bodi itawanasa wanaopiga chenga kurejesha mikopo**



Ukurasa 13

Wananchi wanahitaji kujua ukweli kuhusu tiba wanapoumwa na nyoka




Ukurasa 14

**Uchaguzi unapokaribia, Pwani mguu sawa kufunza wapigakura**


Nipashe

# TESA

Jumanne Septemba 24, 2024

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI


ELIMU

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Pombe na dawa zinazolevya janga linaloangamiza vijana

TUNAJIULIZA itakuwaje mbona Watanzania hawa hasa wa kiume wanajitumbukiza kwenye uvivu, ulevi wa pombe, bangi na dawa za kulevya kupindukia?

Vipi miaka ijayo kama wanaotegemewa kuzalisha au nguvukazi wameumizwa na ulevi, wazalishaji watakuwa wa namna gani, iwapo vijana wengi wa umri kati ya miaka 20 hadi 45 wamekuwa walevi na waraibu?

Moja ya athari kubwa kwa vijana Tanzania, ni unywaji pombe uliokithiri. Kawaida wakazi wengi vijijini na mijini wapo wanaokunywa pombe aina mbalimbali.

Leo kuna pombe ambazo vijana wanachangamkia kupindukia mfano sungura, kadhalika, usambazaji pombe kwa kutumia vifungashio venye ujazo mdogo na kwa gharama ndogo umeshika kasi na unawahamasisha vijana kunywa zaidi kwa bei poa.

Kuwapo vyanzo vya mapato kwa serikali hasa ambavyo haviumizi walipakodi na wananchi kwa ujumla ni jambo jema lakini tunapotafakari suala la ulevi huu vijana wengi wanaathirika sana kwa kiwango cha taifa kuelekea pabaya.

Mbali na pombe, changamoto nyingine ni dawa za kulevya zikiwa pacha wa ulevi kwa vile vinatumiwa na vijana wengi.

Uzoefu unaonyesha kuwa kijana akishazoea dawa zinazolewesha kuziacha inakuwa kizaazaa. Kuna wakati serikali ilijitahidi kudhibiti kwa kiasi kikubwa, matumizi ya dawa zinazolewesha kwa kuhakikisha haziingizwi nchini lakini bado ni tatizo.



Mzuka wa pombe. **PICHA MTANDAO**

Nijitolee mfano wakati nikiwa kijana kabla na baada ya kuanza shule niliona wanaokunywa pombe walikuwa watu wazima wenye familia, hakuna kijana asiyekuwa na familia mke na watoto angeweza kuruhusiwa kujumuika nao.

Hata kama, angekuwa ameoa lakini bado hajawa na uzoefu wa kutosha kimaisha na kuonyesha uelekeo unaokubalika na jamii, haikuwa rahisi kukaa pamoja na watu wazima, kwa mifumo kijadi au kimila ilikuwa imezuia vijana kutojitosa kwenye pombe bila ya kujijengea msingi imara kumudu maisha yake na familia.

Nyakati hizi maisha ni kidijitali, kisiasa, kisaikolojia, kiteknolojia, kimaendeleo hadi kusema kila mtu yuko huru kufanya anavyotaka ili mradi amefikisha umri wa miaka 18 au zaidi.

Hali hiyo inakinzana na sheria, kanuni pamoja na mifumo ya kiroho aliyoiweka Mungu. Kadhalika, serikali kwa dhamira ya kupata mapato zaidi ikapunguza bei ya pombe. Kimsingi mapato ya serikali yanapoongezeka, kwa namna moja au nyingine, yanatarajiwa huduma za kijamii ziboreshwe na kuimarishwa. Hata hivyo pombe haijaweza kuleta mafanikio kimapato.

Operesheni iliyofanywa na Mamlaka la Kuzuia na Kudhibiti Dawa za Kulevya kati ya Agosti 24 na Septemba 2024 imedhihirisha kuwa upo udhaifu mkubwa katika mifumo ya kudhibiti uagizaji na uingizaji dawa hizo.

Ripoti yake inayotolewa mwezi huu, inaonyesha kiasi kikubwa cha dawa hizo zilizoingizwa na kukamatiwa Manispaa za Kinondoni na Ubungo kwa kuwanasa watuhumiwa kadhaa.

Swali linabaki je, dawa hizo zimepitia wapi bila kugundulika mpaka zikawa mitaani kiasi hicho?

Kadhalika, matumizi ya bangi pia yamekuwa yakiongezeka kila kukicha je, Watanzania tunakwama wapi hadi taifa kushindwa kudhibiti matumizi ya dawa zinazolevya?

Katika hali hii isiyoridhisha kuna hofu kuwa huenda vijana wanaokua wakatumbukia kwenye janga hili, nini hatima ya Tanzania?

Tukitafakari tunawaza, Tanzania ya kesho na viongozi wajao watakuwa wa namna gani, wenye mwelekeo gani, je watakuwa na maarifa yapi?

Je, vijana wataishi maisha ya namna gani kama mwelekeo wao kwa sasa ni kunywa na kulewa kupindukia na uraibu?

Mwezi uliopita jijini Dar-es-Salaam, karibu na Posta ya Zamani, nilishuhudia vijana watano wanaume wanne na binti mmoja wamejibanza wakinywa kwa kupokezana.

Vilevile, walikuwa wanavuta sigara moja kwa kupokezana. Nimebakia na maombi, Mwenyezi Mungu uwarehemu vijana hawa na wengine wa aina hiyo maana wanaangamia kwa kukosa maarifa, akili zao zimepinda.

Mungu amewapa utashi kuhusu cha kufanya ili kuwa na uchaguzi sahihi mathalani, ufanye nini, ule au unywe nini, uvaaje au uishi maisha gani?

Hivyo, inabidi kuwajibika kwa maisha dunia moja, 'binadamu wote sawa' lakini tunatofautiana katika uwezo wa kufanya maamuzi sahihi kuishi, vizuri bila kukengeuka hadi kupoteza 'afya ya akili' zetu.

Ombi langu kwa serikali, kunywa pombe kupindukia ikiwemo pia dawa zinazolevya si jambo jema kwa taifa. Ni kitisho.

Hatua madhubuti zichukuliwe kuanzia sasa kwa kupandisha bei za vileo vyote bila kujali vifungashio na ukubwa pia kuhakikisha dawa hizo zinadhibitiwa kwa juhudi zote.

Lengo ni kuokoa, nguvukazi ya taifa, vilevile, atakayethibitishwa kisheria kufanya biashara haramu adhabu kali itolewe na sheria nichukue mkondo wake bila kuoneana haya wala huruma ili tusiendelee kuliangamiza taifa kwa maslahi binafsi.

Taifa bora linahitaji vijana imara, wenye nguvu, afya na akili timamu pamoja na maarifa ya zama zilizopo.

**INAENDELEA UK.13**

ELIMU

NA DK. REUBENI LUMBAGALA

# Kwa kutumia TEHAMA bodi itawanasa wanaopiga chenga kurejesha mikopo

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) inawapa mikopo wanafunzi wenye sifa na pia kukusanya fedha zilizokopeshwa kutoka kwa wanufaika hao wanapohitimu masomo.

Bodi inasisitiza kuwa ni wajibu wa mwombaji kuzingatia kuwa fedha anazokopeshwa kugharamia masomo yake zinapaswa kurejeshwa ili ziwakopeshe wengine wenye uhitaji ili kuongeza idadi ya wasomi katika taasisi hizo na kuchagiza maendeleo.

Tangu 2004 bodi hiyo inawapa wanafunzi wenye uhitaji hasa wanaotoka familia zenye kipato kidogo mikopo kutimiza ndoto za kufikia elimu ya juu.

Ni fedha za kugharamia ada, chakula, malazi, vitabu na mafunzo kwa vitendo kwa makubaliano ya kurejesha fedha hizo baada ya kuhitimu na kuwa na shughuli za kuwaingizia kipato iwe ajira rasmi au za kujiajiri na ujasiriamali.

Mikopo inatolewa si tu kwa wanafunzi wa shahada bali pia wanavyuo wa stashahada wanaosoma kozi za vipaumbele kama afya, ualimu hasa sayansi na ufundi, usafirishaji, nishati, madini, masuala ya tiba, kilimo na mifugo.

Kazi ya kutoa mikopo kwa waombaji haina changamoto kubwa ikilinganisha jukumu la kukusanya fedha zilizotumika kusomesha.

Maana wahenga walisema kukopa harusi, kulipa matanga. Kukusanya mikopo kutoka kwa wanufaika wake umekuwa na changamoto ikizingatiwa kuwa baadhi ya wahitimu hasa waliojiajiri kutojitokeza kulipa mikopo yao kwa hiari si jambo jepesi.

Tena baadhi ya wanufaika bado wana mtazamo kuwa wanapaswa kurejesha mikopo pale tu watakapoajiriwa kwenye sekta rasmi kama vile serikalini au ofisi binafsi, ndipo watakapoanza kulipa kupitia makato ya mishahara.

Hivyo, wapo wanufaika wanaodhani mnufaika wa mkopo wa elimu ya juu hapaswi kulipa mkopo wake kupitia ajira yake binafsi kama vile mama na babalishe, bodaboda, fundi uashi, seremala na mfugaji.

Huu ni mtazamo potofu. Lakini, pia wapo wachache wanaodhani pesa za umma hazina mwenyewe, wakifanya juhudi za kukwepa kulipa deni licha ya kwamba wapo ndugu zao wanaotegemea kupata fedha hizo.

HESLB wanasisitiza kuwa iIli mradi mnufaika anayo shughuli ya kumwingizia kipato iwe ni ajira rasmi yenye mshahara au shughuli binafsi za kujiajiri zinapompatia kiasi fulani cha fedha kwa siku au wiki, analo jukumu la kulipa deni.



Wahitimu wakifurahia mahafali. **PICHA: MTANDAO**

> Ili kuongeza ufuatiliaji kutoka kwa mwanafunzi ambaye amehitimu masomo na ana kipato lakini bado hajaanza kurejesha mkopo uliotumika kumsomesha.

Anatakiwa kutenga fedha kwa ajili ya kupunguza deni lake kwa kulipa kupitia malipo ya serikali yanayofanyika kupitia ‘control number’ iliyoko kwenye taarifa ya mkopo. Lengo ni kufanikisha kupata fedha na kuwawezesha waombaji wengine kupata mikopo kwa miaka mingine mingi ijayo.

Hivyo basi, kwa kutambua ugumu wa kukusanya fedha hasa kutoka kwa wanufaika waliojiajiri na wenye vipato halali, Bodi ya Mikopo imekuja na mfumo wa kisasa wenye kuhusisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA.

Kwa njia hiyo waombaji wameunganishwa kwa kuwashirikisha wadau wengine muhimu kusaidiana kuwabaini wadaiwa mahali walipo na kuongeza makusanyo.

Kwa kushirikiana na kuongeza makusanyo bodi itakuwa na uwezo wa kukopesha waombaji wengi zaidi ikizingatiwa kuwa kuna ongezeko kubwa la waombaji wenye sifa hasa wanaomaliza kidato cha sita ambao wanahitaji mikopo kugharamia masomo yao vyuoni.

Mapema mwezi huu (Septemba 11, 2024), Bodi ya Mikopo ilibadilishana hati za makubaliano na taasisi tatu ambazo ni Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA.

Aidha, kipo chombo cha Credit Information kuongeza wigo wa kuwasaka wadaiwa na kuongeza mapato kwa ushirikiano.

Katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dk. Bill Kiwia anasema: “Katika kazi yetu ya kukusanya fedha za mikopo, tunawahitaji wadau hawa...

Hivyo tunaomba mtufikishie ujumbe kwa wateja wetu kuwa sasa tunakwenda kufanya kazi na washirika watatu na wengine tutawatangazia siku chache zijazo. Tunalenga kuwafikia wadaiwa wote kwa kutumia mifumo.”

Ni ukweli kuwa bodi ya mikopo haiwezi kufanya kazi peke yake na wakafanikiwa bila kushirikisha wadau na kutumia mifumo ya kieletroniki hasa ikizingatiwa maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia yaliyopo sasa.

Na ndiyo maana kazi imehama kwenye utendaji wa kutumia mifumo ya kielektroniki badala ya makaratasi kwa kiwango kikubwa ili kuongeza ufanisi na ubora wa utendaji kazi.

Pamoja na hayo ni nia ya serikali kuwa ni lazima mifumo isomane ili kurahisisha kazi na kuongeza uwazi na uwajibikaji, nidhamu ya fedha na matumizi kwenye majukumu ya kuwahudumia Watanzania. Kwa mujibu wa Dk. Kiwia, hadi sasa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 600 inapaswa kurejeshwa kutoka kwa wanufaika waliosoma katika vyuo mbalimbali.

“Mikopo ambayo imeshaiva ni Sh. trilioni 2.1 na hadi sasa zimerejeshwa Sh. trilioni 1.5, bado bilioni 600 hazijarejeshwa, hivyo kama ilivyo kwa kampeni za urejeshwaji mikopo, tunaunganisha mifumo ili kuwafikia wanufaika wenye kipato waanze urejeshaji,” anasema Dk. Kiwia.

NIDA wanatarajiwa kusaidia kupatikana taarifa za makazi na mawasiliano ya wanufaika wa mikopo, hivyo, bodi ya mikopo itakuwa na uwezo wa kuchukua taarifa muhimu za mnufaika wa mkopo kupitia taasisi hiyo.

Ili kuongeza ufuatiliaji kutoka kwa mwanafunzi ambaye amehitimu masomo na ana kipato lakini bado hajaanza kurejesha mkopo uliotumika kumsomesha.

Aidha, RITA ina jukumu la vizazi na vifo ambapo watakuwa kiungo kupitia mfumo wa kielektroniki kurahisisha wanafunzi kufanya mchakato wa mikopo kwa ufanisi.

Sanjari na hilo, Taasisi ya Credit Info Tanzania inafanya jukumu la kifedha la kukusanya taarifa za wakopaji wa benki na taasisi nyingine za kifedha, na hivyo mteja kabla hajaomba mkopo ni lazima apitie Credit Info.

Kwa mujibu wa Benki Kuu (BoT) inazitaka taasisi zote za fedha nchini kutafuta taarifa za mkopaji kutoka Credit Info kabla ya kumkopesha ili kujua historia ya mkopeshwaji.

Hivyo basi, Credit Info, inawajibika kufanikisha na kuwezesha mchakato wa ukopaji na urejeshaji mikopo kupitia jukumu lake la msingi la kuchakata taarifa za waombaji kupitia benki.

Kwa mantiki hii, endapo bodi ya mikopo itapeleka taarifa za wanufaika wake ambao ni wadaiwa sugu Credit Info, kunaweza kusababisha wadaiwa wa bodi ya mikopo kukosa mikopo kwa sababu hawakopesheki kwenye taasisi mbalimbali za kifedha.

Huu utakuwa ni usumbufu kwao kukosa mikopo, kwa hiyo, ni muhimu kulipa deni la bodi ili kukopesheka kwenye taasisi nyingine za kifedha.

Vilevile, Septemba 13, 2024, Bodi ya Mikopo ilibadilishana hati za ushirikiano TRA kwa lengo la kubadilishana taarifa ili kuboresha utoaji na urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika wake.

HESLB inafafanua kuwa kupitia TRA inaweza kutambua changamoto mbalimbali na hivyo kuboresha huduma zake.

***Mwandishi ni mwalimu wa Sekondari ya Mlali iliyoko Dodoma.***
***Maoni: 0620 800 462***

ELIMU
NA MWANDISHI
WETU

# Wananchi wanahitaji kujua ukweli kuhusu tiba wanapoumwa na nyoka



MAJIRA ya kiangazi yanakaribia na wanaoishi karibu na vichaka na misitu ndiyo msimu wa nyoka kutoka mapangoni na kurandaranda.

Nyoka wapo na watu wanaumwa ndiyo maana, aghalabu ukisafiri kwenye mabasi ya masafa kuelekea au kutoka mikoani unakutana na wauza 'mawe ya kuondoa sumu ya nyoka'.

Ni vipande vyeusi vya mawe ambavyo wengi wananunua bila kujua ni dawa au ni mazoea, hata hivyo, ni mambo yanayoachwa nyuma na sayansi ya kidijitali ya matibabu kwa walioumwa na nyoka.

Wafanyabiashara hao wanatangaza ndani ya vyombo vya usafiri kuwa ukiumwa na nyoka kwangua halafu bandika jiwe kunyonya sumu na ikimalizika litandoka. Unachotakiwa kufanya likianguka ni kuliloweka kwenye maziwa kulisafisha ukiendelea kulitunza kwa matumizi ya siku nyingine.

Aidha, wapo wanaosema ukigongwa na nyoka usipotumia jiwe hilo au Shilingi 50 ama 100 kuondoa sumu mwilini, unaweza kupoteza maisha ikichukuliwa kama huduma ya kwanza.

Kadhalika, wataalamu hao wa mitaani wanasisitiza kuwa ni lazima kutoa meno ya nyoka yaliyobaki mwilini kwa kuchana na wembe au kisu kikali hata mkasi kuyakwangua na kuyaondoa.

Wanaosema hayo wanaelekeza zoezi liwe la haraka kwani baadhi ya meno ya nyoka kama kifutu au kobra (koboko) yakibaki mwilini, ni hatari, husafiri kupitia mishipa ya damu na kufika moyoni maelezo ambayo pengine hayana ukweli.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kuumwa na nyoka wenye sumu kunaweza kusababisha kupooza, kupumua kwa shida na wakati mwingine kukatwa kiungo iwapo sumu itaenea mwilini.

Mbali na hilo, kama sumu itasambaa zaidi na aliyeumwa asipata matibabu anaweza kupoteza maisha, kwa hiyo hatua zingine zinapaswa kuchukuliwa mara moja wakati unapoumwa na nyoka.

Lakini, WHO haizungumzii kubandika jiwe au kukwangua kidonda kama sehemu ya huduma ya kwanza.

Kwa mujibu waMamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), nyoka hatari zaidi Tanzania ni koboko au cobra, ambaye akikuuma usipopata tiba haraka unaweza kupoteza maisha.

Kobra huyo anayepatikana Tabora na ukanda wa magharibi kama Mwanza na Shinyanga, wapo pia kwenye misitu mingi ikiwamo ya Udzungwa.

Anaelezwa kuwa ana sumu kali inayoumiza moyo na nyingine mishipa ya fahamu na ndani ya dakika chache majeruhi anaweza kufariki dunia.

Sasa cha kujiuliza aliyeumwa na mnyama huyu anaweza kutumia jiwe la nyoka na kupona?

### CHA KUFANYA UKIUMWA

Shirika la Habari la BBC linafafanua mambo kadhaa ya kuzingatia, likisema jambo la kwanza usitembee wala kukimbia, kaa kimya na kutulia na ikiwezekana usinyanyue sehemu iliyogongwa iwe mkono au mguu.

Kwa ajili ya kuzuia kusambaza sumu kunakotokana na kukimbia au kutembea. Aidha, usafiri utumike kumpeleka majeruhi hospitalini na kama ni kijijini abebwe bila kupoteza muda, ili kuokoa maisha yake.

Pia, majeruhi na anayemsaidia kumpa huduma ya kwanza wakae mbali na nyoka wasijaribu kukamata.

Iwapo majeruhi umevaa saa, mkufu, vikuku, bangili au nguo ya kukubana eneo ulipoumwa na nyoka vivuliwe mara moja.

### USIYOTAKIWA KUFANYA

BBC inaonya usiweke bandeji kwa nguvu wakati umeumwa na nyoka, hata kama imefungwa, ilegezwe kidogo.

Kumbuka kuwa kama bandeji imefungwa na kukazwa sana, sumu inaweza kuenea kwenye jeraha na sehemu hiyo kukatwa kwasababu ya 'kuoza'.

Usiende kwa waganga wa kienyeji au kutumia dawa yoyote ya mitishamba au nyingine isiyojulikana kama umeumwa na nyoka, kwa hiyo aachana na mawe ya nyoka.

Usitumie kinywaji cha aina yoyote kwanza hadi utakapomuona daktari. Aidha, madai kuwa kuua nyoka au kutumia barafu kunaondoa sumu, yote hayo sio ya kweli.

Wakati ukiumwa na nyoka mwenye sumu, matibabu sahihi ni muhimu ili kuokoa maisha ya majeruhi.

Katika hali nyingine, kifo au uharibifu wa kudumu wa kimwili unaweza kutokea ikiwa hautibiwi mara moja au kama aliyeumwa hatapata matibabu sahihi.

Kwa hivyo usisikie au kutumia njia zingine za matibabu ya kuua nyoka, kuweka barafu kwenye jeraha au hata mbinu nyingine za kijadi zinazopendekezwa.

### EPUKA HAYA

Usikwangue wala kunyonya sumu kutoka kwa mtu aliyeumwa na nyoka, ni hatari unaweza kuwa na vidonda mdomoni ukajiua kwa 'kula' sumu hiyo.

Lakini pia usiikwangue na kuichana ili kutoa meno sehemu iliyoumwa na nyoka.

Wakati wote kumbuka kuwa usiende kwa waganga wa kienyeji anza kwanza na dawa za hospitalini. Usisafishe wala kupaka chochote kwenye sehemu iliyogongwa na nyoka.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani, watu wanaofanya kazi katika kilimo na watoto ni waathirika wakubwa wa nyoka.

Watoto ndio walioathirika zaidi na sumu ya nyoka na kwa ujumla matukio hayo hupatikana duniani kote, lakini kiwango cha vifo katika visa kama hivyo ni kikubwa katika nchi za Kusini-Mashariki mwa Asia ikiwa ni pamoja na India.

Ripoti ya serikali ya India, inasema matukio ya kugongwa na nyoka ni ya kawaida zaidi katika vijiji na maeneo ya mijini.

Aidha, inaeleza kuwa kuna aina zaidi ya 250 za nyoka nchini India, kati ya hizo nyoka 52 wana sumu kali wakiwamo kobra na nyoka wa baharini.

## Pombe na dawa zinazolevya janga linaloangamiza vijana

INATOKA UK.11

Kumbukeni kumcha Mungu ndiyo chanzo cha maarifa na taifa lenye hofu ya Mungu hutenda haki kwa wote na kuuchukia uovu.

Vijana jiulizeni vipaumbele vyenu ni nini? Ni wazi mojawapo ya majibu ni kuwa raia hodari, kujenga familia bora za wacha Mungu mkichangia maendeleo ya nchi.

Acheni kuhadaika na utandawazi, mifumo-dijitali na kuiga yasiyofaa ni wazi mnatakiwa kutafakari njia zenu na kubadilika.

Inavyoelekea mataifa yaliyoendelea hayajali chochote yanafanya kulingana na matakwa yao, hasa yakichochea maovu mfano, kuhamasisha ndoa za jinsia moja au ushoga kwa wanaume na usagaji kwa wanawake na kutunga sheria za kuruhusu kutoa mimba na kuchochea wanawake wasipate ujauzito.

Nyakati hizi hali imekuwa tofauti kiasi cha vijana kuona kuwa kuoa na kuzaa watoto ni dhiki kubwa au kama ni laana, wakati ni baraka au zawadi kuwa na familia. Tambueni vijana kuwa maisha ya wazee wetu yalikuwa yameegamia kwenye misingi na mifumo ya kijadi, kiutamaduni wakiabudu miungu mingine ingawa walifahamu yupo Mungu Muumbaji.

Niwakumbushe vijana wetu hususani wa kiume, wasijisahau kuwa ni wanaume wanaotegemewa kujenga familia zilizobora na endelevu.

Nimekuwa nikisikia msemo dunia inawayawaya ukimaanisha binadamu wanakosa utulivu na umakini kwa kuhangaika huku na huko bila kujua mustakabali wa maisha.

Ukitafakari hali hiyo utagundua kuwa vijana wa kiume kutumbukia kwenye ulevi, hakika ni matokeo ya kuhangaika na ya dunia zaidi kuliko kusimama imara kwa msingi na maadili.

ELIMU
NA SABATO KASIKA

# Uchaguzi unapokaribia, Pwani mguu sawa kufunza wapigakura




Mjumbe wa NaCoNGO mkoani Pwani, Prisca Ngweshemi (kushoto), akishiriki jukwaa. **PICHA: SABATO KASIKA**

MWAKA huu ni wa uchaguzi wa serikali za vitongoji na vijiji pamoja na mitaa maeneo ya mijini, ukitarajiwa kufanyika Novemba 27, kisha utafuatiwa na uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani, Oktoba mwakani.

Kabla ya uchaguzi huo mkuu ambao wapigakura wanawachagua rais, wabunge na madiwani kwa upande wa Bara, Zanzibar wanawachagua marais wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano, wabunge, wawakilishi na madiwani, kuwaandaa wapigakura ni kipaumbele mijini na vijijini.

Kabla ya kufikia hatua hiyo michakato mbalimbali inaendelea, ikiwamo kuboresha daftari la kudumu la wapigirakura, jukumu linalofanywa na Tume Huru ya Uchaguzi ya Taifa (INEC) na ZEC.

Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), nalo linakumbushwa kutoa elimu ya mpigakura kwa wananchi ili wajue umuhimu wa kushiriki uchaguzi kuwapata viongozi wanaowataka.

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Simon Nickson, akiongea kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, anayesema

> Tunategemea mashirika yasiyo ya kiserikali kushirikiana nasi kukabiliana na changamoto zinazoikabili jamii, hasa uelewa kuhusu uchaguzi.

hayo, hivi karibuni, katika mkutano wa jukwaa la mashirika yasiyo ya kiserikali mkoani humo.

Ni kutokana na umuhimu wa elimu hiyo kwa wananchi, anasema mkoa huo unayahimiza mashirika yasiyo ya kiserikali kutoa elimu itakayowajengea uwezo wa kutoa maoni mbalimbali na kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu.

Nickson, anasema elimu ya mpigakura inamsaidia mwananchi kuelewa kuhusu kushiriki mchakato wa uchaguzi kwa kuchagua au kujitokeza kuomba kuchaguliwa kuwa kiongozi.

"Tunategemea mashirika yasiyo ya kiserikali kushirikiana nasi kukabiliana na changamoto zinazoikabili jamii, hasa uelewa kuhusu uchaguzi," anasema Nickson.

Anafafanua kuwa mashirika hayo pia yana jukumu la kuunganisha wananchi, kwa sababu wakati wa kampeni za uchaguzi kuna mambo mengi yakiwamo kuhasimiana kutokana na itikadi za kisiasa.

"Kwa hiyo pamoja na majukumu mbalimbali mlio nayo, kushiriki kutoa elimu ili kusaidia wakazi wa Pwani kujua haki yao kwenye uchaguzi ni jambo muhimu," anasema.

Aidha, Nickson anasisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya mashirika hayo na serikali na pia kati yao ili kurahisisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

"Kuleta maendeleo kunahitaji ushirikiano hata katika uchaguzi, kwa ajili ya kupata viongozi bora watakaoisaidia nchi kuendelea kusonga mbele. Ili kufikia hatua hiyo, elimu ya mpigakura kwa wananchi ni ya muhimu ili waweze kushiriki kwa wingi katika uchaguzi, wachague viongozi sahihi wa kuendelea kusimamia nchi vizuri," anasema.

Mjumbe wa NaCoNGO mkoa wa Pwani, Prisca Ngweshemi, anasema mkoa huo una zaidi ya mashirika 30 yasiyo ya kiserikali, na kwamba yale ambayo hayafanyi kazi kikamilifu, 'watayaamsha'.

Anasema baraza hilo linatamani mashirika yote ya kiraia mkoani humo yawe hai na kufanya kazi kikamilifu, ili kusaidiana na serikali kuwaletea wananchi maendeleo.

"Hivyo, tutayaamsha mashirika yaliyolala kwa kuyafuatilia kujua chanzo ya kutofanya kazi ili iwe rahisi kwetu kuchukua hatua za kuyasaidia kurudi kwenye majukumu yaliyofanywa yakaanzishwa," anasema Prisca.

Prisca anafafanua kuwa baraza lao linatekeleza majukumu mbalimbali ikiwamo kulinda maslahi ya AZAKI, kujenga mitandao na mashirikiano miongoni mwa mashirika yasiyo ya kiserikali na kuwa sauti ya umoja kwenye masuala yao.

"Nchi ina mikakati na mipango iliyojiwekea hasa maendeleo, hivyo nasi ni muhimu kuwa miongoni mwa wadau wanaochangia katika hilo, kwa kuhamasisha wananchi kushiriki shughuli mbalimbali," anasema.

Adha, anaongeza kuwa katika kipindi cha kutekeleza majukumu yao mwaka 2024 hadi hadi 2027 watahakikisha kama kulikuwa na mapungufu kwenye baraza lililopita, wanayarekebisha.

Prisca anasema wamejipanga kusaidia mashirika yasiyokuwa ya kiserikali katika nyanja mbalimbali ikiwamo kuyajengea uwezo mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kitaasisi na kiutendaji.

"Tunataka kusaidia mashirika kuzingatia sheria na taratibu za nchi, kuimarisha ushirikiano kati ya serikali na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, kuimarisha ushiriki wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali katika kuchangia maoni kwenye Dira ya Maendeleo ya 2050," anasema.

Anasema, wamepanga kuongeza juhudi kutekeleza mipango ya taifa kama Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, mikakati mbalimbali ikiwamo kuelimisha wananchi kujua umuhimu wa kujenga taifa lao na kuwa na Tanzania bora kwa Watanzania wote.

Mjumbe anasema baraza lao linatamani kila asasi ya kiraia na wananchi washiriki katika kutoa maoni kwenye dira hiyo ili iwe jumuishi.

Anafafunua kuwa, maendeleo hayo jumuishi, ni katika ushiriki wa makundi maalum kwenye shughuli za kiuchumi na huduma za jamii ili upewe kipaumbele kwenye utekelezaji wa afua mbalimbali za kiserikali na wadau wengine.

"Vipaumbele vya baraza letu katika kipindi cha kutekeleza majukumu yetu kwa mwaka 2024 hadi ifikapo mwaka 2027 ni kurekebisha mapungufu yote ya baraza lililopita na kuja na vingine vipya."



# Halmashauri ya Ikungi yatenga milioni 600/- mikopo 10%

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida imetenga Sh.milioni 600 kwa ajili ya mikopo ya asilimia 10 ya wanawake, vijana na wenye ulemavu ili kuwainua wananchi kiuchumi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Haika Massawe, alisema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya utengenezaji bidhaa mbalimbali za wajasiriamali yakiwamo mafuta ya kupaka, sabuni na vipodozi yaliyofanyika katika Kijiji cha Ikungi chini ya wawezeshaji kutoka Chuo cha Arizona kilichoko Dar es Salaam wakishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi.

Massawe alisema kuwa mafunzo hayo ni chachu kwao kuongeza ufanisi kuweza kujiajiri na hata kutengeneza vikundi ili halmashauri kuwawezesha pindi dirisha la fedha hizo litakapofunguliwa waweze kukopeshwa.

Aidha, Masawe aliwataka maofisa maendeleo jamii katika kata zote za halmashauri hiyo kutimiza majukumu yao kama walivyojaza kwenye barua zao za ajira, ili kuhakilisha wananchi wanapata huduma zote zinazostahili kutoka kwao.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Richard Kabaka, aliwapongeza washiriki wa mafunzo hayo kwa kujitokeza kwa wingi na kuwataka kwamba elimu waliyoipata waiendeleze kwa kuwafundisha wengine ili kuwa na wajasiriamali wengi.

Katika hatua nyingine madiwani wa kamati ya uchumi wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri wa Wilaya ya Ikungi, Ally Mwanga, wamewataka wataalamu wa kilimo kuweka utaratibu mzuri kwa wakala wa mbegu na mbolea ili zifike mapema na kwa wakati wa msimu wa kilimo.

**Massawe alisema kuwa mafunzo hayo ni chachu kwao kuongeza ufanisi kuweza kujiajiri na hata kutengeneza vikundi ili halmashauri kuwawezesha pindi dirisha la fedha hizo litakapofunguliwa waweze kukopeshwa.**

# Matumizi mbolea ya ruzuku yaongezeka tani 34,000

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

MATUMIZI ya mbolea ya ruzuku inayotolewa na serikali, yameongezeka kutoka tani 500,000 kwa mwaka 2022/23 hadi tani 840,000 mwaka 2023/24.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Laurent Joel, aliyasema hayo jana alipokuwa akifunga mafunzo ya siku mbili kwa vijana wa Mradi wa Jenga Kesho iliyobora (BBT) eneo la Chinangali wilayani Chamwino.

Alisema ongezeko hilo linaonesha kuwapo na mwamko mkubwa wa matumizi ya mbolea kwenye kilimo na kwamba itawabadili wakulima kutoka kilimo cha mazoea na kuwa cha kisasa chenye tija.

"Matumizi ya mbolea ya ruzuku yameongezeka, TFRA inazidi kupanua wigo wa utoaji elimu ya matumizi ya mbolea kwenye kilimo," alisema Joel.

Hata hivyo alisema kampeni ya utoaji elimu ya matumizi ya mbolea itaendelea kutolewa ili kuongeza idadi ya watumiaji wa mbolea kwenye kilimo.

Aidha, aliwahimiza wakulima wa maeneo mbalimbali nchini kuendelea kujisajili kwenye mfumo ili watambulike na kupata mbolea ya ruzuku.

Aliwapongeza vijana wa BBT kutokana na mafunzo waliopata ambayo yatawajenga katika kilimo wanachotarajia kufanya.

Alisema mafunzo ya siku mbili yaliyotolewa na TFRA kwa vijana wa BBT yana maana kubwa katika kilimo wanachojiandaa kufanya kwa msimu wa kilimo.

Mkurugenzi huyo aliiwashukuru Wizara ya Kilimo kutokana na kuwalea vizuri vijana wa BBT jambo linalochangia kuzidi kukua kwa kilimo hapa nchini.

Naye Mratibu wa BBT, Mathed Kahaya aliwashukuru TFRA kwa mafunzo waliyotoa, huku akisema isiwe mara ya kwanza bali waendelee kwenda kutoa mafunzo kwa vijana wa BBT.

Alisema kutokana na dhamira ya vijana hao kuleta mapinduzi kwenye kilimo ili Tanzania iweze kujitosheleza kwenye mazao ya chakula na biashara na kuuza nje ya nchi, matumizi ya mbolea yanapaswa kuzingatiwa ili kuwa na kilimo chenye tija.



Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki, Dk. Pius Chanya, akizungumza jana kwenye mkutano wa hadhara na wananchi wa Kijiji cha Chicheho, Kata ya Sanza kuhusu umuhimu wa kushiriki kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu pamoja na uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura utakaoanza mkoani Singida Septemba 25, mwaka huu. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Bil. 62/- zatengwa kuwapa mitaji wajasiriamali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Bodi ya Mfuko Self, Paul Samgawe, amesema serikali imetenga Sh.bilioni 62.4 kwa mwaka 2024/25 kwa ajili ya kuwakopesha wajasiriamali mitaji kupitia mfuko wa Self.

Alisema hayo jana jijini hapa katika halfa ya kukabidhiwa ofisi Mtendaji Mkuu mpya wa mfuko huo, Santeli Manongi.

Samgawe alisema wamejipanga kuhakikisha wanaongeza kasi ya utoaji huduma ili kuwafikia wananchi wengi.

Alisema lengo ni kuhakikisha wanatekeleza maono ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha taasisi hiyo inawawezesha wananchi na kuendelea kutoa gawio kwa serikali kila mwaka kutokana na faida inayopatikana.

"Lengo la serikali kuanzisha taasisi hii ni kuhakikisha inatoa mikopo kwa ajili ya kuwawezesha wananchi mikopo yenye riba nafuu. Niwasihi mwendelee kutoa huduma kwa ufanisi ili lengo liweze kutimia," alisema.

Aliongeza kuwa: "Mmefikia mtaji wa Sh.bilioni 62 hakikisheni fedha hizo zinatumika kuongeza wigo wa utoaji huduma kutoka mikoa 14 sasa mfike nchi nzima."

Aidha, alimpongeza Mtendaji Mkuu mpya kwa kuteuliwa na kumtaka kuhakikisha kuwa taasisi hiyo inapanua wigo wa utoaji huduma ya mikopo kwa wananchi.

"Lazima mhakikishe kuwa mnapanua wigo wa bidhaa ambazo mfuko mnazozitoa lakini riba za mikopo zinapungua bila kuathiri mtaji wa mfuko," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko huo, Santeli Manongi, alisema atahakikisha wanaendelea kuboresha kasi ya utoaji huduma kwa wananchi.

Vile vile, aliahidi kuendelea kulinda fedha zilizopo na kuziendeleza ili waweze kuzalisha faida zaidi.

"Maono niliyonayo ni kuhakikisha tunafanya kazi kwa bidii na kuwa taasisi bora tutafikia maono kwa kuzingatia kuwa tuna jukumu la kuhakikisha tunawafikia wananchi wote," alisema.

Naye Ofisa Mtendaji wa Mfuko anayemaliza muda wake Mudith Cheyo alisema katika kipindi cha miaka sita ya uongozi wake wamefanikia kuongeza wigo wa utoaji huduma kutoka mikoa sita hadi 14.

Alisema hadi sasa mfuko imekua sana ambapo ina mali za thamani ya Sh.bilioni 68 na mtaji wa bilioni 62.6 na mikopo iliyopo kwa wateja ni Sh.bilioni 54.6 na madeni ya taasisi ni Sh. bilioni 7.8.

Alisema hadi sasa mfuko unajiendesha wenyewe na umekuwa ukitoa gawio kwa serikali kila mwaka kiasi cha Sh. milioni 200.



## Serikali yafafanua matibabu bure wajawazito, watoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KAIMU Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, Joseph Endrew, amesema huduma za wajawazito na watoto umri chini ya miaka mitano zinatolewa bure kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya serikali.

Alisema hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Makambako, Deo Sanga, baada ya baadhi ya wananchi wa Kata ya Makambako kuomba ufafanuzi juu ya sera ya msamaha wa matibabu kwa wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

"Kama mwongozo wa serikali unavyosema mjamzito anapofika kwenye kituo akabainika kama yeye ni mjamzito akapewa kadi ya kliniki kuanzia pale huduma zinazohusiana na ujauzito wake atahudumiwa bure hadi kipindi cha kujifungua na mtoto kuanzia umri sifuri hadi miaka mitano huduma zote ambazo siyo za kibingwa wanapata bure," alisema Endrew.

Hivyo aliwataka wananchi hao pindi wanapohudumiwa wawe na risiti za matibabu ambayo wanapewa ili wawabaini wahusika wanaokiuka sera hiyo.

Pia alisema katika mwaka wa fedha 2024-2025 Halmashauri ya Mji wa Makambako imetengewa Sh. milioni 763 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la upasuaji, chumba cha kuhifadhia maiti, majengo la kulaza wagonjwa katika hospitali ya mji iliyopo Mlowa na kununua vifaa tiba kwenye zahanati.

Awali wakizungumza katika mkutano huo, wananchi hao walisema licha ya sera kueleza kuwa wajawazito na watoto waliopo chini ya miaka mitano wanatakiwa kupewa matibabu bure bado wengi wao wamekuwa wakiambiwa walipie hela hasa wanapohitaji dawa licha ya kupata vipimo bure.

Baadhi ya wananchi hao, akiwamo Zaituni Kawambwa aliomba serikali kuja na ufafanuzi sahihi kuhusiana na adha hiyo ili kuondoa malalamiko yaliyopo ambayo wataalamu wa afya wameendelea kupewa kwa madai ya kuwa hawafuati sera hiyo.

"Kwa asilimia kubwa vipimo vipo vizuri lakini sasa shughuli kwenye dawa unaweza ukapewa dawa aina moja nyingine ukaambiwa ukanunue duka la dawa," alisema Kawambwa.

Naye Dominika Lugusi alisema ni vema serikali ikabainisha pia ni huduma zipi ambazo zinatolewa bure kwa wajamzito ili kuondoa sitofahamu hiyo.

Mbunge wa Makambako, Deo Sanga aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa wakati pindi wanapokutwa na matatizo hayo.

# TBS yatoa hadhari ununuzi wa bidhaa pasipo kuhakiki

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limewataka wananchi kuhakikisha wanasoma kwa makini taarifa za vifungashio kwenye bidhaa kabla ya kufanya ununuzi.

Lengo ni kujiridhisha endapo bidhaa hizo zimethibitishwa ubora na hazijaisha muda wake wa matumizi pamoja na taarifa zingine za msingi kwa lengo la kulinda afya zao.

Ofisa Masoko wa shirika hilo, Deborah Haule, alitoa tahadhari hiyo wakati wa mwendelezo wa kampeni ya elimu kwa umma illiyotolewa mkoani Kigoma. Wananchi 2,730 pamoja na wajasiriamali 110 walifikiwa.

Alisema lengo la kampeni hiyo ni kuelimisha wananchi kuhusiana na umuhimu wa kutumia bidhaa zilizothibitishwa ubora, jinsi ya kutoa taarifa za bidhaa hafifu pamoja na zile ambazo hazijaisha muda wake wa matumizi.

Alisema kupitia kampeni hiyo, serikali kwa kutambua mchango wa wajasiriamali katika kukuza uchumi wa nchi na uchumi wao binafsi inathibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha bure.

Deborah alisema mashirika ya viwango ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) yameingia makubaliano, kwamba bidhaa ikishapimwa na kuthibitishwa na shirika la viwango la nchi husika, ikivuka mipaka na kwenda nchi nyingine haitakiwi kupimwa tena.

"Kwa hiyo, hii ni fursa nzuri kwa wajasiriamali wanaothibitisha bidhaa zao wanachotakiwa ni kuja na barua ya utambulisho kutoka Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) hatutaki kumwacha nyuma mjasiriamali yeyote," alisema.

Alisema TBS inatoa elimu hiyo kwa lengo la kuwajengea wananchi uelewa kuhusu umuhimu wa viwango ili kulinda afya za walaji na kuwawezesha wazalishaji bidhaa kihimili soko la ndani na nje ya nchi.

Alisema matakwa ya ubora ni pamoja na bidhaa kuwa na tarehe ya mwisho wa matumizi, hivyo kupitia kampeni hiyo wanaelimisha jamii na wadau kuhusu taarifa za kuzingatia kwenye vifungashio kabla ya kununua bidhaa.

Deborah alisema elimu hiyo inatolewa kwa wananchi kupitia maeneo ya wazi, ikiwamo minadani, vituo vya mabasi, masoko na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya watu wengi.

Ofisa Udhibiti Ubora wa TBS, Peter Musiba, aliwataka wafanyabiashara kujitokeza kusajili vyakula na vipodozi ili kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa kukidhi matakwa ya sheria za nchi na kulinda afya za walaji.



Balozi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya, Chifu Rocket Mwashinga, akitoa mchango wake mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kilichokuwa kimeitishwa na Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Christina Mndeme. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Imani potofu chanzo wanawake kutotumia uzazi wa mpango

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wanawake katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanadaiwa kuacha kutumia njia za uzazi wa mpango kutokana na imani potofu wakiamini kuwa njia hizo zina madhara kwao na kwa watoto.

Mratibu wa Afya ya Uzazi ya Mama na Mtoto wa Halmashauri ya Mbeya, Nitike Kyejo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akitoa taarifa ya tathmini ya matumizi ya njia za uzazi wa mpango.

Kikao hicho cha tathmini kiliwahusisha maofisa afya kutoka katika halmashauri mbalimbali za Mkoa wa Mbeya, watoa huduma za afya ya mama na mtoto na wakuu wa idara ya afya wa halmashauri za mkoa huo.

Aidha, kikao hicho kilikuwa na lengo la kupata uzoefu kutoka kwa waratibu wa afya ya mama na mtoto wa Halmashauri ya Chamwino mkoani Dodoma ambao inadaiwa kuwa wamefanya vizuri kwenye uhamasishaji wa matumizi ya njia hizo kutoka asilimia 22 mpaka 92.

Nitike alisema baadhi ya wanawake hao wamekuwa wakiamini kuwa wakitumia njia hizo huwa inasababisha ugumba na hivyo wanaamua kuachana nazo hali ambayo inawasababishia kushindwa kupanga uzazi kwenye familia zao.

"Wengine wanaamini kuwa wakitumia kitanzi watoto wanazaliwa wakiwa wameshikilia vitanzi hivyo, kwa hiyo imani hizi zimekuwa zikikwamisha hamasa ya matumizi ya njia za uzazi wa mpango kwenye maeneo yetu," alisema Nitike.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kwa njia mbalimbali ili waondokane na imani hizo potofu ambazo zinasababisha mpangilio mbovu wa uzazi.

Alisema wanatumia vyombo vya habari kutoa elimu pamoja na kuwafuata wananchi kwenye maeneo yao na kwamba wanawafuata hata mashambani wanakofanya shughuli zao za uzalishaji.

Mratibu wa Shirika la JHPIEGO ambalo linaratibu hamasa hiyo, Waziri Njau alisema wanaendelea na juhudi mbalimbali za kuhakikisha elimu inawafikia wananchi kwa kiwango cha juu ili waondokane na imani potofu.

Alisema wanaendelea kuwaunganisha waratibu wa uzazi wa mama na mtoto katika halmashauri na wadau mbalimbali wa afya ili kuhakikisha huduma hiyo inaimarishwa nchini.

Alisema wanashirikiana pia na baadhi ya mashirika yakiwamo ya kimataifa yanayohusika na masuala ya afya ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma wanayostahili.

"Huduma za uzazi wa mpango ni muhimu sana katika kupangilia watoto kwenye familia, kwa hiyo niwahakikishie kwamba tutaendelea kushirikiana ili kufanikisha hili," alisema Njau.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Daliwason Andrew, alisema wameweka utaratibu wa kuhakikisha kila mwanamke anayekuwa amejifungua anapata elimu ya uzazi wa mpango ili alee vizuri mtoto wake.

Alisema elimu hiyo inatolewa kwa mume na mke ili wachague wenyewe njia ambayo wataona wao ni rahisi kuitumia badala ya kumpatia mwanamke pekee.

Serikali inahamasisha matumizi ya uzazi wa mpango ili kuondoa tatizo la wananchi kuzaliana bila utaratibu na kuwapa wanawake muda wa kupumzika kutoka uzazi mmoja mpaka mwingine pamoja na kupata muda wa kuwalea watoto wao kabla ya kupata wengine.



**HABARI ZANZIBAR**

# Serikali yatoa ufafanuzi ushirikiano ZARI, TARI

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema taasisi mbili zinazojishughulisha na masuala ya utafiti ZARI kwa upande wa Zanzibar pamoja na TARI kwa Tanzania Bara zinafanya kazi kwa ushirikiano katika masuala ya utafiti, lengo likiwa ni kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo na uzalishaji.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis katika Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe Ameir Abdalla Ameir.

Ameir alitaka kujua ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili katika masuala ya utafiti.

Akijibu swali hilo, Shamata alisema ushirikiano ulipo umejikita katika maeneo tofauti ikiwamo katika kufanya kazi za utafiti katika upande wa magonjwa yanayoathiri maendeleo ya sekta ya kilimo ikiwamo muhogo na mpunga.

Alisema kwa muda mrefu yapo maradhi yanayoathiri ukuaji wa mazao ya muhogo na hivyo kusababisha kupungua kwa uzalishaji wake na hivyo wakulima kushindwa kupata mavuno mazuri.

Aidha, alisema ushirikiano na taasisi hizo kumesaidia katika upatikanaji wa mbegu bora ambazo zimeleta mafanikio kwa wakulima.

**Ameir alitaka kujua ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili katika masuala ya utafiti.**

Akifafanua zaidi, Shamata alisema wakulima hivi sasa wamepatiwa mbegu za kisasa zinazokwenda na wakati wa uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi baada ya mbegu nyingi za asilia kupotea.

Alisema hivi sasa wamekuwa wakifanya utafiti kuhakikisha kwamba mbegu za asili za mazao mbalimbali maarufu zinapatikana kwa ajili ya kuleta matokeo mazuri.



Meneja Mradi wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Sylivia Daulinge, akizungumza kuhusu uzinduzi wa kampeni mpya inayozingatia ubora wa elimu jumuishi kwa wanafunzi wa shule za umma, inayolenga kumsomesha mtoto wa kike. Kulia ni Ofisa Msaidizi wa TAMWA, Cleopatra Ngesi. **PICHA: BEATRICE MOSES**

## Mkongo chini ya bahari kubadilisha ikolojia ya kidijitali

**Na Gwamaka Alipipi**

IMEELEZWA kwamba mkongo wa chini ya bahari wa 2Afrika wenye urefu wa kilomita 45,000 unakwenda kubadilisha ikolojia ya kidijitali nchini, kuleta mchango mkubwa katika maendeleo.

Mkongo huo ulizinduliwa mwaka jana na Rais Samia Suluhu Hassan katika kituo cha mkongo wa mawasiliano baharini-Airtel Cable Landing Station kilichopo maeneo ya Mbezi Beach jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika mkutano wa Connect 2 Connect wa mwaka 2024 jijini Arusha, Mhandisi Mkuu wa mtandao wa Airtel Tanzania, Dk. Adedoyin Adeola, alisema watashiriki katika harakati za kubadilisha sekta ya kidijitali nchini kupitia kuwashwa kwa kituo hicho.

Alisema miundombinu hiyo mipya ya mkongo mpya wa mawasiliano wa chini ya bahari utachangia kuinua na kubadilisha sekta ya kidijitali nchini kupitia mtandao wa intaneti ulioimara ambao kwa sasa unatumiwa na watu bilioni tatu duniani.

"2Afrika italeta miundombinu muhimu ya intaneti na kuunganisha watu takribani bilioni 1.2 na zaidi. Umuhimu wa mkongo huu ni kutokana na uwezo wake wa kuleta mabadiliko ya kipekee katika upatikanaji wa huduma za kidijitali Afrika, kuchochea ukuaji wa kiuchumi, kuongeza usawa na kuchangia katika ubunifu wa kiteknolojia," alisema.

Alisema hatua hiyo itaiweka Afrika katika nafasi nzuri ya kuunganishwa na uchumi wa kidijitali wa dunia ambao ni jumuishi, wezeshi na endelevu.

Dk. Adeola alisema mkongo huo unaiweka Tanzania katika nafasi ya kuwa kitovu cha teknolojia katika ukanda wa Afrika Mashariki na barani Afrika.

Alisema kituo cha mkongo wa bahari wa 2Afrika utakuwa daraja litakaloziba ufa wa mgawanyiko wa kidijitali kati ya maeneo ya mijini na vijijini kwa kuboresha upatikanaji wa intaneti na kuendesha ukuaji wa biashara za mtandaoni, kuchochea ongezeko la vyanzo vya mapato kwa serikali na kuboresha maisha ya wananchi.

Mkurugenzi wa Biashara wa Airtel Tanzania, Joseph Muhere, alisema Airtel inaunga mkono safari ya mabadiliko kuelekea uchumi kamili wa kidijitali kupitia miundombinu ya hali ya juu ambayo iko sambamba na maono ya taifa ya kuchangia katika ukuaji wa kiuchumi na kijamii pamoja na ujumuishwaji wa kidijitali.

## Mfumo kudhibiti upotevu fedha za umma wazinduliwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ), Said Seif Said amesema Mfumo wa Pamoja wa Kidijitali kwa Serikali (SGES), utaimarisha utendaji wa serikali kwa kutoa huduma za kidijitali.

Aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa mfumo huo wa kutoa mawasiliano kwa simu Zanzibar, ambapo (eGAZ) kwa kushirikiana na kampuni kwa huduma za kidijitali Tanzania Tigo Zante zitashirikiana katika uendeshaji wa mfumo huo.

Lengo ni kuleta mageuzi ya huduma za serikali, kujenga uchumi wa kidijitali ulio wazi na wenye ufanisi katika kusimamia maendeleo ya miundombinu ya ICT kwenye sekta za umma Zanzibar.

Alisema mfumo huo pia utasaidia kuzuia upotevu wa fedha kwenye taasisi za umma katika utoaji wa huduma za msingi kwa njia ya kidijitali na kuimarisha utendaji wa serikali kwa kutoa huduma hizo.

Alisema mamlaka hiyo imefanya tathmini na kubaini uwepo wa njia moja ya matumizi hayo kwa taasisi za serikali ambao utasaidia upotevu wa Sh. milioni 50 kwa siku sawa na Sh. bilioni 18 kwa mwaka kutokana na taasisi hizo kutumia mifumo tofauti.

Aidha alisema mamlaka hiyo inafanya jitihada za makusudi kuhakikisha inapunguza gharama na kuongeza makusanyo serikalini kwa kuzitaka taasisi mbalimbali kujiunga na mfumo huo ili kuepusha upotevu wa mapato hayo.

"Mfumo huu wa kisasa utaimarisha utendaji wa serikali kwa kutoa huduma mbalimbali za kidijitali kama vile ujumbe mfupi wa maneno, ujumbe wa pamoja, huduma USSD, majukwaa ya SMS ya mwingiliano, na Kituo cha Data cha hali ya juu," alisema.

Hata hivyo alisema lengo la mfumo huu ni kurahisisha mawasiliano, kuboresha utoaji wa huduma, kuongeza ushirikishwaji wa umma kwa taasisi za serikali na mkakati wa serikali mtandao wa mwaka 2023-2027.

Akizungumzia udhibiti wa mianya ya upotevu wa fedha serikalini alisema mamalaka hiyo inafanya tathmini mara kwa mara katika taasisi za umma kuhakikisha mapato ya serikali hayapotei kwa kuweka mifumo imara yenye uwezo wa kurekodi kila hatua anazozifanya mtumishi.

Mkurugenzi wa Tigo-Zantel Kanda ya Zanzibar, Aziz Said Ali, alisema kampuni hiyo inajivunia kuwa mshirika mkuu katika mradi huo wa kimapinduzi wenye dhamira ya kusaidia mabadiliko ya kidigitali ya serikali.

Alisema mfumo wa Pamoja wa Kidigitali kwa Serikali (SGES) utaimarisha miundombinu ya kidijitali ya serikali na kuhakikisha huduma zinatolewa kwa ufanisi, uwazi na kupatikana kwa urahisi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**GODWIN ACKO MSEKWA,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Sita chenye index S0149-0945 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Sekondari Rungwe Mwaka 2019, Yeyote atakaeikiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/CHE/41556/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**JASTIN LAWI KIMANGA** anatangaza kupotea kwa Passport ya kusafiria yenye namba **TAE 699631** iliyotolewa na makao makuu PCO DAR ES SALAAM mwaka 2024. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/32737/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**BRENDA BENEDICT CHALE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0265-0007** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **CORNELIUS GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2011. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR /UBU/196875/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SOPHIA JEROME CLEMENT** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1773/0058** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MIEMBESABA SECONDARY SCHOOL mwaka 2015. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/PWA/KIB/19428/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JUDI JOSEPH NDIMI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya SANLG yenye usajili namba **MC 953 EFS,** CHASSIS NAMBA: **BPKM3H2T1PK014436** na ENGINE NAMBA: **KL16FMJ230914436.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/LON/35540/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA TRACTOR

**IAN BENJAMIN MOSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya **TRACTOR** aina ya **GREEN DEER** yenye usajili namba **T 952 DGF,** CHASSIS NAMBA: **PY5503E006762** na ENGINE NAMBA: **PY3029T239266.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/ILA/204304/2024**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI NAMBA 38 YA 2024**

**WINFRIDA WILLIAM WILLIAM............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **AUBI MTASIWA..............................MJIBU MAOMBI**
2. **NATHANIEL ADAM KICHULUMBI....MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**GROLIA KALINGA**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 17/10/2024 mbele ya Mwenyekiti E. MOGASA wewe mwenyewe au mtume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 17 mwezi September, 2024.

E. MOGASA
MWENYEKITI.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO MJINI**

**KITUO CHA MJINI MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...59/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: MOSHI SALUM MBEGHA wa MASIKA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA YAHYA PASSCIENCE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24 Mwezi 10 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 23 mwezi 09 mwaka 2024

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Mirathi Na 1490/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**AYOUB ABDALLAH MWABONDO WA.....................**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**WA MIRATHI YA MAREHEMU YALIYOLETWA NA**
**HUSNA ABUBAKARI MLEWA**
**ABDALLAH AYOUB MWABONDO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za uzimamizi wa mirathi katika mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 04 mwezi 10 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Imetolewa leo tarehe 20 mwezi 09 mwaka 2024

HAKIMU

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 22470 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**AIDANO DASTAN MNKABENGA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY STEPHEN MHINA MNKABENGA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 17th day of October 2024

Dated at Korogwe this 20th day of September 2024

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA 7 LA MWAKA 2023**

**(kutokana na uamuzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya . Asilia kutoka Baraza la kata Bitimanyanya -chunya)**

**GERVAS KIBABA.......................................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**MERE NDALAMA................................MRUFANIWA**

**KWA: MERE NDALAMA**
**POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Unataarifiwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa mahakama binafsi au wakili wako tarehe 24/09/2024 siku ya Jumanne saa 3:00 kamili asubuhi. Bila kukosa. ELEWA KWAMBA, Ukikosa kufika siku hiyo, shauri litasikilizwa bila wewe kuwepo na uamuzi utatolewa.
Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 09/09/2024

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

---


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/ PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Maelfu wajitokeza mazishi viongozi Hezbollah

**BEIRUT,** Lebanon

MAELFU ya wananchi nchini Lebanon wamejitokeza kwenye mazishi ya kuwaaga viongozi wawili wa kundi la Hezbollah Ibrahim Aqil na Ahmad Mahmoud Wehbi, ambao waliuawa Ijumaa katika shambulio la Israel.

Ilielezwa kuwa mazishi hayo yalifanyika katika viunga vya kusini mwa Beirut, ambayo ni ngome ya Chama cha Mwenyezi Mungu.

**Tuko pamoja na upinzani wa Kiislamu, tunafuata maamuzi ya Hassan Nasrallah. Inatoa nguvu zaidi, na kile kilichotokea jana usiku ni mwanzo tu wa jibu.**

Kiongozi namba mbili wa kundi hilo Naïm Kassem, alisema kuwa umati huo wa watu waliojitokeza na kusimama mbele ya jeneza la Ibrahim Aqil na Ahmad Mahmoud Wehbi ni ishara ya kuipinga Israeli.

"Suluhu la kijeshi la Israel halitawarudisha waliokimbia makazi yao kutoka kaskazini hadi makwao na kutatua tatizo lao. Ili kufanya hivyo, watalazimika kwenda Gaza na kusimamisha vita. Vitisho havitutishi. Na hatuogopi hali mbaya zaidi. Tumeingia katika awamu mpya ya vita," alisema.

Ilielezwa kuwa inawezekana awamu mpya tayari imeanza kwa shambulio la kwanza la Hezbollah katika maeneo ya kijeshi huko Haifa, nchini Israel, huku wafuasi wa Hezbollah wakifunga safu nyuma ya kiongozi wao asiyepingwa Hassan Nasrallah.

"Tuko pamoja na upinzani wa Kiislamu, tunafuata maamuzi ya Hassan Nasrallah. Inatoa nguvu zaidi, na kile kilichotokea jana usiku ni mwanzo tu wa jibu," alisema Hassan Moqtad, mfuasi wa Hezbollah, katika umati huo.

Aidha, ilielezwa kuwa kuongezeka kwa mivutano kwa vyovyote vile kunazua hofu ya kutokea vita kamili nchini Lebanoni. Huku Jeshi la Israel likiwashauri raia wa Lebanoni kujiepusha na maeneo yanyolengwa ya Hezbollah kusini mwa Lebanoni, ikieleza kuwa mashambulizi yanayolenga kundi hilo yataendelea katika siku za usoni na yatakuwa makubwa na sahihi zaidi.

Wakati huo huo, ilielezwa kuwa utafutaji wa miili katika vifusi vya jengo lililolengwa na shambulio la Israel bado unaendelea, huku waokoaji wakiendeleza shughuli hizo, wakati familia za wahanga zikisubiri kupatikana kwa miili ya wapendwa wao.

Wizara ya Afya ilitangaza kwamba itatumia vipimo vya DNA ili kutambua baadhi ya maiti. **RFI**

## Mageuzi ya UN yaidhinishwa

**NEW YORK,** Marekani

NCHI wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) zimeidhinisha kwa kauli moja mkataba wa mustakabali wa umoja huo licha ya pingamizi la Russia na mataifa mengine.

Uamuzi huo ulifanyika jana baada ya baraza kuu la umoja huo linalohusisha nchi wanachama kukutana New York nchini Marekani kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali yanayohusu mustakabali UN.

Rais wa baraza kuu la Umoja wa Mataifa Philemon Yang, alithibitisha kuidhinishwa kwa mkataba huo wa UN kuhusu mustakabali wa baadaye, licha ya kupingwa na Russia na mataifa mengine mengi.

Ilielezwa kuwa mpango huo unakuja katika kiwingu cha kuwapo mgawanyiko mkubwa miongoni mwa jamii ya ulimwengu, na kwamba ilipangwa kuwa makubaliano hayo yataidhinishwa kwa kauli moja na nchi zote 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa bila ya kupigiwa kura.

Hata hivyo, baada ya mazungumzo yaliyoendeshwa kwa kipindi cha miezi kadhaa, Russia ilionesha kusababisha mivutano kabla ya mkutano huo wa kilele wa siku mbili.

Vile vile, ilielezwa kuwa nchi wanachama wameuidhinisha mpango huo licha ya Russia kulazimisha ufanyike mchakato wa kupigwa kura kuhusu kile kinachoitwa mkataba wa mustakabali wa baadaye.

Pia kwa mujibu wa wajumbe wa Russia, Belarus na Nicaragua, awali zilishatishia kujitenga na hatua ya kuidhinisha mpango huo katika mkutano huo wa kilele. Na kwamba mkataba kuhusu mustakabali wa Umoja wa Mataifa ulijadiliwa chini ya uongozi wa Ujerumani na Namibia.

Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, alitoa wito wa kufanyika mageuzi katika taasisi hiyo ya kimataifa pamoja na mashirika mengine ya kimataifa ili kuifanya jumuiya hiyo kuwa na uwezo zaidi wa kuchukuwa hatua katika kukabiliana na migogoro mingi na vita na kuwezesha ulimwengu kuwa mahala pa haki. **TRT**



Rais wa Kenya, William Ruto, akisalimiana na kikosi cha Jeshi la Polisi la taifa hilo lililotumwa nchini Haiti kuimarisha usalama, baada ya kuwatembelea nchini humo juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Muswada wawamulika wakulima Kenya

**NAIROBI,** Kenya

MUSWADA mpya ulio bungeni nchini Kenya, unalenga usajili wa wakulima wote wa mazao ya mboga wadogo kwa wakubwa na kwamba iwapo utapitishwa, watahitajika kutumia vifaa vya kilimo kutoka kwenye chanzo kilichosajiliwa.

Ilielezwa kuwa hatua hiyo itajumuisha wakulima wanaozalisha hasa maua, matunda, mboga, mimea ya mapambo na dawa.

Muswada huo wa Sheria ya Mamlaka ya Mazao ya Mimea ya 2024, unasema kuwa mtu sharti awe na leseni ili aweze kusindika, kuagiza nje au kuuza nje bidhaa za mboga.

Wafanyabiashara hao pia watalazimika kujisajili na serikali za kaunti zinazosimamia shughuli zao bila malipo.

Ilielezwa kuwa wauzaji wa nje na waagizaji watatakiwa kupata leseni kutoka serikalini ili kushughulikia mazao mbalimbali. Na kwamba watakaokiuka hiyo wanaweza kutozwa faini ya kati ya shilingi milioni moja hadi mbili au kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu.

"Mtu hataruhusiwa kuweka mazao yake kwa biashara ya ndani ya nchi isipokuwa kama amepewa leseni na serikali ya kaunti husika," muswada huo ulisema.

Muswada huo pia unalenga kuanzisha ushuru wa mazao ya bustani kwa mauzo ya nje na uagizaji wa bidhaa kutoka nje, ambako ushuru wa mauzo ya nje utatozwa asilimia 1.5 kwa mazao au bidhaa yoyote ya mboga.

Mazao yaliyowekwa kwenye makopo, chupa za kuhifadhia yaliyokaushwa au yale yanayoletwa viwandani kwa ajili ya kuhifadhiwa katika makopo au chupa hayatalipishwa ushuru. **TRT**

## Trump: Nikishindwa sitawania tena urais

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa zamani wa Marekani, Donald Trump, amesema hatawania muhula wa nne mfululizo wa urais ikiwa atashindwa kwenye uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika katika taifa hilo Novemba 5, mwaka huu.

Kiongozi huyo wa upinzani aliyasema hayo katika mahojiano aliyofanyiwa na chombo kimoja cha habari cha nchini humo.

Akiulizwa ikiwa anaweza kugombea tena katika miaka minne ijayo iwapo hatafanikiwa katika kuwania kiti cha urais kwa mara ya tatu mfululizo, rais huyo wa zamani mwenye umri wa miaka 78 alimwambia mwandishi wa habari wa Marekani Sharyl Attkisson: "Sidhani kwamba hilo litatokea kabisa. Tunatumai tutafanikiwa."

Trump anakabiliwa na ushindani mkubwa dhidi ya mshindani wa Chama cha Democrat Makamu wa Rais wa Marekani Kamala Harris, huku kura ya maoni ikionyesha ushindani mkali kati ya wagombea hao wawili katika majimbo ambayo yanaamua mshindi wa uchaguzi, licha ya kuwa Harris anaonekana kuongoza katika kura ya maoni kwenye ngazi ya taifa. **VOA**

# KOCHA AZAM ASEMA TIMU YAKE BADO HAIJAKAA SAWA

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya ushindi wa bao 1-0 juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam dhidi ya Coastal Union, Kocha Mkuu wa Azam FC, Rachid Taoussi, amesema kikosi chake bado kinahitaji marekebisho kwani hakijakaa sawa, huku akikiri pamoja na kupata pointi tatu hakikucheza vizuri.

Akizungumza na wanahabari baada ya kumalizika kwa mchezo huo, alisema yote hayo yanasababishwa na kutokuwa na muda mrefu wa kukifundisha kwani wamekuwa wakikaa masaa machache kabla ya kucheza michezo mingine.

**"Tunahitaji saa 72 za kupumzika kabla ya mchezo mwingine, hivi wachezaji wangu wanachoka sana, nadhani ndiyo maana leo hawakucheza vizuri kabisa licha ya kwamba tumepata ushindi," alisema kocha huyo.**

Alisema tatizo aliloliona kwenye mchezo wa juzi ni wachezaji wake kupoteza sana mipira, kushindwa kupambana kuwania mipira inayoanguka na kushindwa kukabiliana na mawinga hatari na wenye kasi wa Coastal Union.

"Hatukucheza vizuri, tulipoteza sana mipira, hata ya kugombea hatukuwa tunaipata, pamoja na kwamba hatutengeneza nafasi nyingi, lakini tumefunga bao moja tu kitu ambacho nafasi chache zilizopatikana tungeweza hata kupata mabao mawili au matatu.

Nadhani sababu kubwa ni ile ile, hatuna muda wa kupumzika, tunapumzika masaa machache kabla ya kucheza mchezo mwingine," alisema kocha huyo ambaye alianza kukifundisha kikosi hicho hivi karibuni akichukua nafasi ya Youssoupha Dabo.

Naye Kaimu Kocha Mkuu wa Coastal Union, Joseph Lazaro, alisema tatizo lilianza waliporuhusu bao la mapema.

"Mpango wangu nilipanga tusifungwe bao la mapema, badala yake tukaruhusu mapema zaidi kuliko siku zingine zote, kwa hiyo mpango wangu haukufanikiwa.

"Baada ya wao kupata bao hawakucheza tena kwenye mpango wao, walionekana wanashambulia kwa ungalifu sana, lakini zaidi walikuwa wanazuia.

"Hii imetuweka kwenye wakati mgumu sana, watu wanasema tumecheza vizuri, mimi kama kocha siwezi kusema tumecheza vizuri halafu tumepoteza, kwa hiyo tuna kazi ya kufanya," alisema.

Bao pekee la mchezo huo liliwekwa wavuni na Nassor Saadun dakika ya tisa na kupeleka Azam hadi nafasi ya tatu ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi nane.

## Tabora United yaomba radhi mashabiki

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa Klabu ya Tabora United, umewaomba radhi mashabiki na wadau wa timu hiyo kutokana na matokeo yasiyoridhisha waliyoyapata katika mechi tano walizocheza mpaka sasa.

Tabora United imecheza michezo mitano, kati ya hiyo imeshinda miwili, kupoteza miwili na kutoka sare mchezo mmoja.

Ofisa habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala, juzi alisema matokeo waliyoyapata kwenye uwanja wao wa nyumbani kwa kupoteza hayajawafurahisha na yamewaumiza.

Alisema hata hivyo, timu yao ina kikosi kizuri na bado kuna michezo mingi mbele yao ambayo wana uhakika timu itarejea kwenye mstari na kupata matokeo mazuri.

"Tunawaomba radhi mashabiki wetu na wadau wote, matokeo haya si mazuri, lakini niwahakikishie timu yetu ni nzuri na bado tuna nafasi ya kufanya vizuri, kwa sasa tunaendelea kujipanga kwa ajili ya michezo yetu ijayo," alisema Mwagala.

Alisema kwa sasa timu yao inashika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu na hiyo inawapa hamasa ya kuendelea kupambana kuhakikisha wanabaki kwenye nafasi za juu.

"Tupo nafasi ya nne ingawa kweli kuna baadhi ya timu chini yetu hazijacheza michezo mingi kama sisi, lakini bado hiyo kwetu ni hamasa ya kuhakikisha tunaongeza kasi na kujipanga kufanya vizuri kwenye michezo inayokuja," alisema.

**ACHA HIZO WEWE!...**




Mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland, akikoromeana na beki wa kati wa Arsenal, Gabriel Magalhaes, baada ya straika huyo kumrushia mpira nyuma wakati wa mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Etihad juzi na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

## Mbio za Mbuzi kusaidia jamii na wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU mbalimbali wametakiwa kujitokeza kuzipa sapoti mbio za mbuzi kwa ajili ya kuisaidia jamii wakiwamo wanafunzi wasiojiweza na miradi mbalimbali ya elimu nchini.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mratibu wa mbio hizo, Paul Muhato, baada ya mashindano hayo yaliofanyika katika viwanja vya The Green, maarufu kama viwanja vya Farasi, Oysterbay jijini Dar es Salaam.

Paul alisema lengo la mashindano hayo ni kusaidia jamii huku akiwataka wadau mbalimbali kujitokeza kwa wingi kuunga mkono juhudi za Klabu ya Rotary kuhakikisha wenye shida wanapatiwa ufumbuzi.

"Tuna imani kwamba Mbio za Mbuzi za mwaka huu zimeleta kielelezo cha nguvu ya ushirikiano katika kuchangia maendeleo ya elimu Tanzania.

"Tuna furaha kuwa na Vodacom Tanzania kama mdhamini mkuu na tunawashukuru wadhamini wetu ambao wengi wao wamejiunga nasi kwa mara nyingine tena kwa kuendelea kutuamini na kuungana na sisi katika kuandaa mbio hizi," alisema Paul.

Naye rais wa Klabu ya Rotary, Himanshu Bhattbhatt, alisema mbio za mwaka huu zilizobebwa na kaulimbiu ya 'Carnival,' zimeendelea kufanya yale ambayo yanaitambulisha zaidi Rotary kukutanisha wadau katika kuihudumia jamii.

"Kaulimbiu ya mwaka huu ni wito kwa wadau wote kukutana na kusherehekea ushirikiano wetu na mafanikio ambayo kwa pamoja tumeyapata katika kusaidia jamii," alisema Bhattbhatt.

Mmoja wa washiriki wa mashindano hayo, Clemence Michael, alisema ni mazuri na yana mvuto hivyo aliomba msimu ujao watu waongezeke yawe ya kuvutia zaidi lakini pia waandaaji waongeze zawadi.

Naye mshiriki Sebastian Sagamba, alisema maboresho ya mbuzi yamekuwa mazuri, mabanda mengi, lakini pia michezo ya watoto imeboresha na kuwa yenye mvuto wa aina yake.

Aliomba mwakani yazidi zaidi na wale vijana wanaokimbiza mbuzi wapewe 'tracksuit' ili wawe kwenye mvuto na kupamba mashindano hayo.

Kwa miaka 20 mbio za mbuzi zimekuwa zikiwaleta pamoja wadau katika siku iliyojaa furaha kwa lengo la kuchangia miradi ya kijamii, ikiwa ni moja ya matukio muhimu jijini Dar es Salaam.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MUSIALA ATAKIWA CITY

KLABU ya Manchester City ipo mbioni kumsajili Mjerumani Jamal Musiala, 21, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Real Madrid kwa kiungo huyo wa Bayern Munich. ***(Teamtalk)***

### CALVERT-LEWIN HAKIELEWEKI

MSHAMBULIAJI wa England, Dominic Calvert-Lewin, 27, hajakaribia kusaini mkataba mpya zaidi ya msimu ujao na Everton, huku Newcastle United ikiendelea kufuatilia hali ya mchezaji huyo. ***(CaughtOfiside)***

### ARNOLD NA LIVERPOOL

MKATABA wa mlinzi wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold, 25, unamalizika msimu ujao na mchezaji huyo wa Kimataifa wa England amesema kushinda mataji itakuwa sehemu muhimu ya mawazo yake linapokuja suala la kusaini nyongeza ya mkataba. ***(Liverpool Echo)***

### GYOKERES AVUTIA EPL

KLABU za Arsenal, Chelsea, Liverpool na Tottenham Hotspur zote zinavutiwa na mshambuliaji wa Sporting Sweden, Viktor Gyokeres, 26. ***(Teamtalk)***

### NEWCASTLE NA KOLEOSHO

NEWCASTLE United ndio klabu ya hivi punde zaidi ya Ligi Kuu England kuingia kwenye kinyang'anyiro cha kutaka kumsajili mshambuliaji wa chini ya miaka 21 mzaliwa wa Marekani raia wa Italia, Luca Koleosho, 20, ambaye anawaniwa na Burnley. ***(HITC)***

### USAJILI KUFUNGWA MAPEMA

LIGI Kuu England pamoja na Ligi Kuu za Ulaya, zinajaribu kukubaliana mpango ambao utamaanisha kuwa usajili ujao wa majira ya joto utafungwa kabla ya kuanza kwa msimu. ***(Mirror)***

### POTTER AITAKA EVERTON

KOCHA wa zamani wa Brighton na Chelsea, Graham Potter, angependa kujiunga na Everton ikiwa nafasi itapatikana. ***(Football Insider)***

### LUKEBA AFUATILIWA

REAL Madrid inamfuatilia mlinzi wa RB Leipzig na Ufaransa Castello Lukeba, 21. ***(Marca)***


### YILMAZ ANYATIWA VILLA

KLABU za Aston Villa, Fulham na Nottingham Forest zinamfuatilia winga wa Galatasaray, Baris Alper Yilmaz, 24, wakati Forest, Brighton na Tottenham Hotspur zikimnyatia mshambuliaji mwenza wa Uturuki, Semih Kilicsoy mwenye umri wa miaka 19, ambaye yuko Besiktas. ***(CaughtOffside)***

### DIBLING AFUATILIWA

WAKALA wa kusaka vipaji wa Manchester United, Newcastle na Tottenham walifuatilia mechi ya Jumamosi ya Southampton ambapo kiungo wa kati wa England, Tyler Dibling, 18, aliifungia klabu hiyo. ***(HITC)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA ACHEFUKA KADI NYEKUNDU YA TROSSARD

**MANCHESTER,** England

MIKEL Arteta amesema anatarajia mechi 100 za Ligi Kuu England kutoa angalau kadi moja nyekundu msimu huu baada ya Leandro Trossard kutolewa kwenye mechi ya Arsenal ya sare ya mabao 2-2 dhidi ya Manchester City, Jumapili.

**Erling Haaland alianza kufunga dakika ya tisa, lakini mabao kutoka kwa Riccardo Calafiori na Gabriel Magalhaes yaliwapa wageni uongozi wa 2-1.**

Akiwa tayari ameshapewa kadi ya njano, Trossard alimchezea vibaya Bernardo Silva na kumfanya mwamuzi Michael Oliver kumpa kadi ya pili ya njano mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ubelgiji.

Tukio la Jumapili ni mara ya pili kati ya mechi tatu kwa Arsenal kwa mchezaji wake kupata kadi nyekundu kwa namna hiyo baada Declan Rice kupewa dhidi ya Brighton.

City walitawala kipindi cha pili kwa matokeo hayo na kuambulia pointi moja kupitia kwa mtokea benchini

## ●●● Wavulana walichanganyikiwa sana baada ya mchezo, waliweka moyo na roho zao...

John Stones bao la kusawazisha dakika ya 98.

Katika mchezo huo huo, Jeremy Doku alionekana kukwepa adhabu kwa kuchelewesha kuanza tena kipindi cha kwanza na Arteta alisema: "Hicho ndicho ninachosema. Ni dhahiri kwamba si lazima kutoa maoni juu yake. Ni mara ya pili. Mimi natarajia mechi 100 za Ligi Kuu England kuwa na kadi nyekundu msimu huu."

Alipoulizwa kama anahisi anaruhusiwa kutoa maoni yake ya kweli kuhusu tukio hilo, Arteta alisema: "Leo sitaki."

"Napendelea kutotoa maoni nimeliona na liko wazi, hivyo niwaachie nyie, tayari nilikuwa kwenye matatizo makubwa nikijaribu kutatua kilichotokea uwanjani, si tatizo langu kutatua kinachotokea uwanja."

Arteta alisifu uthabiti wa wachezaji wake katika kipindi cha pili wakati City waliponyanyua mikwaju 20 hadi sifuri kwa Arsenal wakitafuta bao la kusawazisha huku wakiteleza kwa kasi muda ulioongezwa mwishoni mwa mchezo.

"Jinsi timu inashindana haiaminiki," Arteta alisema. "Ninajivunia sana. Huwezi kutupwa katika hali ngumu zaidi dhidi ya mpinzani wa aina hiyo. Jinsi tulivyoshughulikia hali hiyo ilikuwa ya kushangaza. Ninajivunia sana.

"Wavulana walichanganyikiwa sana baada ya mchezo. Walitia moyo sana. Waliweka moyo na roho zao katika kila kitendo. Kisha kuadhibiwa katika dakika ya mwisho - ilikuwa 97 [dakika], kisha 99 [dakika] - walivunjika moyo wanajua pia kwamba wamepiga hatua nyingine kubwa leo kufanya kile ambacho wamefanya kama watu binafsi hapa.

Pamoja na timu hizo kugawana pointi, City wanasalia kileleni kwa pointi 13 baada ya michezo mitano huku Arsenal wakishika nafasi ya nne wakiwa na pointi 11.



# HAALAND AFIKIA REKODI YA RONALDO REAL MADRID

**MANCHESTER,** England

ERLING Haaland ameifikia rekodi ya Cristiano Ronaldo kama mtu mwenye kasi zaidi kufunga mabao 100 kwa klabu moja ya Ulaya, akiwa na Manchester City kwenye sare ya 2-2 ya Ligi Kuu England dhidi ya Arsenal Jumapili.

Bao la mchezaji huyo wa Kimataifa wa Norway katika dakika ya tisa kwenye Uwanja wa Etihad, likizidisha kasi kati ya Gabriel Magalhaes na William Saliba kabla ya kumtungua David Raya, na limemfanya afikishe mabao 100 katika mechi 105 alizoichezea City.

Arsenal ilitangulia dakika za lala salama katika kipindi cha pili, kabla ya John Stones kufunga bao la kusawazisha na kuwaokoa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England.

Mwaka 2011, Ronaldo alifunga bao lake la 100 kwa Real Madrid, pia katika mechi yake ya 105. Mnamo mwaka 2024, Kevin De Bruyne alikuwa mchezaji wa 18 wa Manchester City kufikisha mabao 100, na kupata tuzo hiyo katika mechi yake ya 372 kwa klabu.

Haaland tayari alikuwa amevunja rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi katika mechi nne za msimu wa Ligi Kuu akiwa na tisa, zikiwamo hat-trick mbili.

Mwanzo huo mzuri ulimaanisha kwamba aliingia kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano nyumbani kwa Inter Milan akiwa na mabao 99 katika michezo 103 na akiwa na nafasi ya kuvunja rekodi ya Ronaldo.

Lakini licha ya kupata nafasi kadhaa za kipindi cha kwanza, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, aliachwa akiwa amechanganyikiwa katika sare ya bila kufungana.

# Maresca ammwagia sifa Fofana

**LONDON,** England

ENZO Maresca alimsifu mlinzi Wesley Fofana baada ya Chelsea kushinda mabao 3-0 dhidi ya West Ham kwenye Ligi ya England.

'The Blues' walipata ushindi wa kuvutia kutokana na mabao mawili kutoka kwa Nicolas Jackson na bao la baadaye kutoka kwa Cole Palmer, wakitumia nafasi ya ulinzi mbovu kutoka kwa 'Wagonga Nyundo' hao.

Matokeo hayo yaliashiria ushindi mwingine wa Ligi Kuu England kwa kocha mpya Maresca - ambaye amepoteza mchezo mmoja pekee kwenye ligi hadi sasa msimu huu, dhidi ya Manchester City.

Alikuwa ni beki wa kati Fofana ambaye bosi huyo alimsifu kwa haraka baada ya mchezo.

Nyota huyo wa Ufaransa ameanza mechi zote tano za ligi za Chelsea msimu huu baada ya kukosa sehemu kubwa ya kampeni ya 'The Blues' hao msimu uliopita.


"Wes ni mchezaji ambaye ninampenda sana, ninampenda Wes," alisema Maresca akiwaambia waandishi wa habari baada ya ushindi huo wa Jumamosi.

"Anafanya vizuri baada ya kuumia mwaka mmoja, na kwa mchezaji yeyote duniani, unapokuwa nje kwa mwaka mmoja halafu unarudi si rahisi, na anafanya kiwango cha juu. Hiki ndicho kitu pekee tunachotaka kutoka kwake."

Maresca pia alifichua kuwa uamuzi wake wa kumtoa beki huyo haukuwa kwa sababu ya jeraha na wasiwasi.

"Sababu iliyotufanya kumbadilisha ni kwa sababu tunajaribu kumlinda kidogo," aliendelea. "Pia alikuwa kwenye kadi ya njano. Si jambo kubwa. Kipindi cha pili walimbadilisha [Mohammed] Kudus upande wake na pengine ilikuwa hatari kubwa kumbakisha, lakini hakuna jeraha lolote."





# *Alexander-Arnold ataka kukosolewa*

**LIVERPOOL,** England

MLINZI wa kulia wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold, amesema anakaribisha kukosolewa na kocha Arne Slot ili kuwa beki wa kuogopwa Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, amejizolea sifa kwa ustadi wake wa kushambulia lakini pia amekuwa akiandamwa na simulizi isiyo na urembo kwenye safu ya ulinzi ya mchezo wake. Hata hivyo, akizungumza baada ya ushindi wa mabao 3-0 wa Liverpool dhidi ya Bournemouth Jumamosi, alisema anataka Slot kumsaidia kubadili hilo.

"Nilimwambia Slot kwamba ningependa kuwa beki ambaye hakuna anayetaka kuja dhidi yangu Ulaya," alisema Alexander-Arnold.

"Tulikubaliana kuwa atakuwa mkali kwangu," aliongeza. "Iwapo wakati wowote mshambuliaji ananikaribia na kunipita, ataniita kwenye mikutano, na mikutano ya mtu binafsi na kusema hili haliwezi kutokea.

"Tunapitia kila mchezo pamoja na anaangazia pale anapotaka niboreshe. Hata baada ya mchezo wa Milan.

"Inaburudisha sana kuwa na kocha ambaye atasaidia na kuniongoza na kunifundisha jinsi ya kuwa mchezaji bora.

"Mimi ni mtu ambaye ninataka kujifunza, mtu ambaye anataka kuwa bora na mtu ambaye anajitahidi kuwa bora zaidi."

Alexander-Arnold alikashifu dhana kwamba yeye ni mbovu katika kulinda, ingawa alikiri inaweza kuwa vigumu kuiondoa.

"Nadhani mtazamo huo labda ulikuwa mkali ikiwa nitakuwa mkweli," alisema Alexander-Arnold.

HABARI MICHEZO

## Fadlu: Simba itakuwa tishio

INATOKA UK. 24

mabao zaidi ya manane nimefunga upande wa Kusini, katika kumbukumbu zangu nadhani ni bao moja tu nimefunga upande mwingine, hata mechi na Yanga kule kule," alisema.

Straika wa zamani wa Simba, Freddy Michael ambaye alikuwapo uwanjani, alisema licha ya ushindi, lakini amekoshwa na Ateba, huku akiitabiria kufika mbali.

"Nimekuja kuangalia mechi, nimekuja kuwaona rafiki zangu, unajua kwenye kikosi nina marafiki zangu wengi sana.

"Simba imecheza vizuri, imeshinda, ina wachezaji wazuri, imesajili wachezaji wengi wenye ubora, Ateba ni straika mzuri na amefunga, nadhani wataenda kufanya vizuri msimu huu, nawatabiria fainali," alisema.

Mchezaji na kocha wa zamani, Abdallah Kibaden, yeye alikoshwa na golikipa, Moussa Camara.

"Wasiwasi wangu ulikuwa golini, lakini kumbe tuna kipa mzuri zaidi kuliko wote waliotangulia," alisema.

## Gamondi aanika siri ushindi Yanga

INATOKA UK. 24

wanaelekeza nguvu zao kwenye michezo yao ya Ligi Kuu baada ya kufanikiwa kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunarejea kwenye ligi, lazima tuwe makini kwa sababu ligi si nyepesi, unaweza kuona namna timu zilivyojiandaa, natarajia ushindani mkubwa, akili zetu lazima tuzielekeze huko tukisubiri kujua wapinzani wetu kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Gamondi.

Droo ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika inarajiwa kuchezeshwa Oktoba 7, mwaka huu jijini Cairo, Misri yalipo Makao Makuu ya Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Baada ya droo hiyo wawakilishi wa Tanzania kwenye mashindano hayo, Yanga na Simba zitawafahamu wapinzani wao kwenye michuano hiyo.

Kwa upande wa watani wao wa jadi, Simba ambao wanaiwakilisha nchini kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, nayo imetinga hatua ya makundi baada ya kuitupa nje Al Ahli Tripoli ya Libya kwa jumla ya mabao 3-1, ushindi ambao waliupata katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, hii ikiwa ni baada ya mchezo wa kwanza uliochezwa Libya wiki moja kabla kumalizika kwa sare tasa.

# TIMU 5 BADO HAZIJAONJA LADHA YA USHINDI LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikiingia raundi ya tano, jumla ya timu tano bado hazijaonja ladha yoyote ya ushindi.

Timu hizi ni Prisons, Pamba Jiji, JKT Tanzania, Coastal Union na KenGold, zimecheza michezo tofauti, zikiwa hazijashinda mechi yoyote ya Ligi Kuu msimu huu.

Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu, Prisons ambayo iko nafasi ya tisa kwenye msimamo wa ligi, imecheza michezo minne bila kushinda, ikitoka sare mechi zote na ina pointi nne.

Pamba Jiji, imeshatimiza michezo mitano mpaka sasa ikiwa imepanda daraja msimu huu, lakini haijaonja ladha ya ushindi wa Ligi Kuu, ikitoka sare nne na kupoteza mmoja, ikiwa na pointi nne kwenye nafasi ya 10 ya msimamo.

**JKT Tanzania imecheza michezo mitatu ambayo yote imetoa sare, ikiwa na pointi tatu na inashika nafasi ya 13.**

Coastal Union mpaka sasa imeshacheza michezo minne, ikitoka sare moja tu na kupoteza mitatu, ikikamata nafasi ya 15 na KenGold inayoshika mkia, ikiwa imecheza mechi nne, ikipoteza zote na haijavuna pointi mpaka sasa.

Singida Black Stars ndiyo timu iliyoshinda michezo yote iliyocheza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Timu hiyo imeshinda michezo minne iliyocheza kwenye ligi na kuwa na ushindi wa asilimia 100. Ilianza ligi kwa kuifunga KenGold mabao 3-1, ikaichapa Kagera Sugar bao 1-0, ikapata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya KMC, kabla ya kuifunga Pamba Jiji bao 1-0.



Wachezaji na baadhi ya viongozi wa benchi la ufundi la Simba, wakishangilia baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi Al Ahli Tripoli ya Libya kwenye mechi ya marudiano ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na wenyeji hao kufuzu hatua ya makundi. **MPIGAPICHA WETU**

## *Biashara yaanza biashara asubuhi Ligi Championship*

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Biashara United ilianza vema kampeni yake ya kutaka kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 nyumbani, Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara, dhidi ya Maafande wa Transit Camp, katika mchezo wa raundi ya kwanza Ligi ya Championship iliyoanza wiki iliyopita.

Bao pekee katika mchezo huo lilifungwa na Januari Benson na kuipa pointi tatu mbele ya mashabiki wa timu hiyo.

Wakati Biashara United iliyoshuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu wa 2021/22 ikianza vema, timu ya Polisi Tanzania iliyoteremka msimu wa 2022/23, ilianza vibaya Ligi ya Championship kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Mbuni FC.

Polisi Tanzania pamoja na kuwa nyumbani, Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, ilishindwa kabisa kukabiliana na maafande wenzao wa Mbuni FC wenye maskani yake Arusha na kujikuta ikipoteza nyumbani katika mchezo wa kwanza.

Kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro, wenyeji, Kiluvya FC ya Pwani, walishindwa kuutumia vema uwanja wa nyumbani kwa kukubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Stand United.

Bao la Stand United, timu iliyoshuka daraja msimu wa 2019/20 kutoka Ligi Kuu, lilipachikwa nyavuni na Nassor Idd.

Michezo hiyo ilikuwa inakamilisha raundi ya kwanza ya ligi hiyo, ambapo baada ya kukamilika, Mtibwa Sugar inasimama kileleni baada ya wiki iliyopita kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Green Warriors.

Songea United inashika nafasi ya pili, Mbuni FC ikiwa nafasi ya tatu, Stand United ikikamata nafasi ya nne na Biashara United nafasi ya tano.

# Michezo

Jumanne Septemba 24, 2024

Nipashe




Arteta alia na kadi nyekundu ya Trossard UKURASA 21

MWAMBA HUYU HAPA...



Shujaa wa Simba, Kipa Moussa Camara, akiwalalamikia mabeki wa timu hiyo baada ya kufanya makosa na kumlazimu kufanya kazi ya ziada kuokoa shuti la mshambuliaji wa Al Ahli Tripoli ya Libya, Agostinho Cristovao 'Mabululu', dakika za mwisho wakati wakiongoza kwa mabao 2-1, kwenye mechi ya marudiano ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na wenyeji hao kufuzu hatua ya makundi kwa ushindi wa mabao 3-1. **NA MPIGA PICHA WETU**

# Fadlu: Simba bado, itakuwa tishio zaidi

**Na Adam Fungamwango**

Asifu upambanaji wa wachezaji huku akitaka zaidi, Freddy Fungafunga amkubali Ateba, awatabiria fainali...

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amewaambia wanachama na mashabiki wa timu hiyo ambao wanaonekana kuanza kukisifia kikosi chao baada ya kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, kuwa bado hakijafika pale ambapo yeye anahitaji, akiwaahidi kuwa baadaye kitakuwa tishio zaidi ya hivi wanavyokiona.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo wa mkondo wa pili wa raundi ya kwanza, Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya, Fadlu alisema kikosi chake hakijaimarika vile ambavyo anahitaji, lakini akiwasifu wachezaji wake vijana wasio na uzoefu wa michuano mikubwa kwa kupambana kwa moyo wa kijasiri mpaka kutinga hatua hiyo.

Katika mchezo huo uliochezwa juzi, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Simba ilishinda mabao 3-1 yaliyowekwa wavuni na Kibu Denis, Leonel Ateba na Edwin Balua, yakiipeleka hatua ya makundi kwa jumla ya mabao hayo, baada ya mchezo wa kwanza ugenini nchini Libya timu hizo kutoka suluhu.

**"Tuliruhusu bao, lakini wachezaji wangu hawakuondoka kwenye mpango mkakati, hata wakati wa mapumziko niliwaambia wasiwe na hofu, waendelee kucheza kama ilivyokuwa awali.**

Nina kikosi kipya, wachezaji wengi vijana ni mara ya kwanza kucheza hatua hii, nadhani wamejifunza mengi, namna ya kucheza mechi ugenini, mashabiki wanavyojazana uwanjani na kuwazomea, na vituko vya timu za Afrika Kaskazini," alisema kocha huyo.

Alisema baada ya kutinga hatua hiyo wachezaji wake hasa wale wasio na uzoefu ambao ni wengi kwenye kikosi chake, wataendelea kujifunza hasa kwenye michezo ya makundi, lakini akisema anaendelea kukisuka kikosi chake kuwa tishio.

"Hapa bado, hiki kikosi bado naendelea kukisuka ili kiwe hatari zaidi, naona mashabiki wameanza kuwa na furaha, lakini mimi kama mwalimu bado nina kazi ya kufanya, kitakapofika pale ambapo nahitaji, kitakuwa hakishikiki," alisema raia huyo wa Afrika Kusini.

Wakati kocha huyo akiongea hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, rais wa Heshima na Mwekezaji, Mohamed Dewji, amewasifia wachezaji wa timu hiyo, akisema kwa sasa wana wachezaji wapambanaji wanaopigania nembo ya klabu.

"Tumepitia miaka michache migumu Simba, lakini ushindi wa leo umenifurahisha sana. Vijana ni wapya na wachanga, lakini wamepigana kwa moyo wao wote," alisema Mo.

Mchezaji Kibu Denis yeye alionesha kushangaa mabao yake mengi kuyafunga upande wa Kusini mwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, akisema ana bahati nalo.

Kibu aliyefunga bao la kwanza katika mchezo huo, amesema katika kumbukumbu zake amewahi kufunga bao moja tu lango la Kaskazini mwa uwanja huo.

"Yaani mimi huwa nafunga sana kule sijui kwa nini,

INAENDELEA UKURASA 23

## Gamondi: Hakuna wa kumwogopa makundi

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema matokeo mazuri wanayoyapata yanatokana na mtindo wake wa kubadilisha badilisha wachezaji kwenye kikosi chake cha kwanza.

Jumamosi Yanga ikicheza katika Uwanja wa New Amaan Complex visiwani Zanzibar, ilitinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kutoa kipigo cha mabao 6-0 dhidi ya CBE ya Ethiopia, hivyo kufuzu kwa jumla ya mabao 7-1, kutokana na ushindi wa bao 1-0 iliyoupata wiki moja kabla ugenini.

Akizungumza na Nipashe juzi, Gamondi alisema ugumu wa ratiba ya ligi na mashindano ya kimataifa yanamfanya kutumia wachezaji tofauti tofauti katika kila mchezo.

"Hii ni faida ya kuwa na kikosi kipana, kila mchezaji anayepata nafasi anafanya kile ninachokitarajia, ratiba yetu ni ngumu sana, ni lazima tufanye 'rotation' (mzunguko) ya wachezaji," alisema Gamondi.

Alisema anafanya hivyo ili kuwapa muda wa kupumzika na kujiandaa kwa mchezo unaofuata katika kila ratiba ya timu hiyo msimu huu.

"Naangalia mahitaji ya timu kwa wakati huo, mfano kwenye mchezo wetu dhidi ya CBE kule Zanzibar kuna wachezaji walianzia benchi na kuwapa nafasi wachezaji wengine, nilimtumia Nkane kama beki wa pembeni na alifanya vizuri alipoingia, unaona naweza nikaanza na Nzengeli [Max], Chama [Clatous] na Pacome [Zouzoua], nje wapo akina Aziz Ki, Prince Dube na Musonda, ratiba za michezo yetu inalazimu kufanya hivi," alisema Gamondi.

Katika hatua nyingine, Gamondi, amesema kwa sasa

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >